www.umg.co.tz

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Mwelekeo






**SIASA**

UK.14

**ELIMU**



**Ruangwa yavuka lengo ujenzi shule za sekondari kila kata**

Uk. 12

**MAKALA**

**Ushoga na dhana ya kuoana jinsia moja. Je; ni halali?**

Makala ⇉ Uk.11

Toleo Na. 00004

| Jumatano Machi 8 - 14, 2023 |

umgdigital umgdigital mwelekeo@umg umgdigital



# Samia asafiri na hawa milenia



Dk. Angeline Mabula

Jenista Mhagama

Dk. Dorothy Gwajima

Dk. T. Ackson

Prof. J. Ndalichako

Ummy Mwalimu

Uk. 4


**HABARINDANI**

**Wanawake 27,000 wafanyiwa ukatili**

Uk. 3

**CCM Mbeya yajipanga kusafisha propaganda za wapinzani**

HABARI UK.3



**Liverpool v Man U : Mechi saba za kukumbukwa**

Uk. 21

**HABARINDANI**

**Serikali yasikia kilio cha vikongwe**





HABARI UK.2



**Vijana waitiwa mikopo ya Coaster, Bajaj**

Uk. 3

RIPOTI MAALUM KUTOKA NANYUMBU



Nyumba ya vikongwe Sigele Mtehiya (90) na mumewe, Laisa Mmole (97), wanaodai nyumba zao mbili kuvunjwa (pichani), bila kulipwa fidia kwa ajili ya ujenzi wa barabara. (Picha: Abdul Mitumba, Nangaka, Mtwara.)



Sigele Mtehiya (90)



Laisa Mmole (97)

# Serikali yasikia kilio cha vikongwe

## Ni waliovunjiwa nyumba kupisha barabara

**Na Abdul Mitumba, aliyekuwa Nanyumbu**

SIKU kadhaa baada ya gazeti hili kuripoti habari kuhusu mgogoro kati ya vikongwe waliovunjiwa nyumba zao kupisha ujenzi wa barabara mpya na serikali, Ofisi ya Waziri Mkuu, imesikia kilio hicho na imeanza kuchukua hatua ili kupata majibu ya malalamiko ya wananchi hao.

Mgogoro huo umeibuka miaka saba sasa tangu kukamilika kwa ujenzi wa barabara hiyo ya Mangaka-Mtambaswala inayounganisha Tanzania na Msumbuji.

Katika mgogoro huo, baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Namasogo katika Kata ya Chipuputa, wilayani Nanyumbu, wanalalamikia kile wanachodai kuwa ni kurukwa katika kulipwa fidia.

Wananchi hao wakiwemo vikongwe wawili, Laisa Mmole (97) na mkewe Sigele (90), wamepaza sauti zao wakimuomba Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, awasaidie walipwe haki zao.

Katika malalamiko yao, vikongwe hao pia walimtaja Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuwa awakimbilie na kuwasaidia wakiamini wana haki ya kulipwa tena siyo kwa sababu ya huruma tu.

> **Tuna jukumu la kufuatilia ili tujue nini kimetokea. Tunaamini baada ya muda mfupi ujao, tutapata majibu...**

Kufuatia hali hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu, imesema imeanza kufuatilia malalamiko hayo ili kujua kilichotokea.

Ofisa mmoja katika ofisi hiyo, Andrew Max Makota, alisema tayari wamewasiliana na ofisi ya Meneja wa Wakala wa Barabara (Tanroads) mkoani Mtwara kupata maelezo ya kina kuhusu malalamiko hayo.

"Tuna jukumu la kufuatilia ili tujue nini kimetokea. Tunaamini baada ya muda mfupi ujao, tutapata majibu," alisema Makota akizungumza na mwandishi wa habari hii kwa njia ya simu kutoka jijini Dodoma.

Kabla ya hatua ya sasa, Katibu wa Waziri Mkuu, Raymond Gowelle, alipata fursa ya kuona (clip ya video) ya kikongwe Sigele Mtehiya, akilalamikia kile alichokiita kuwa ni dhuluma aliyofanyiwa na Tanroads.

Katika clip hiyo, kikongwe huyo (pichani), anamuomba Rais na Waziri Mkuu wamkimbile ili wakamsaidie alipwe haki yake.

Hata hivyo, Katibu Gowelle hakusema lolote baada ya kuona malalamiko hayo.

Mwanzoni mwa sakata hili, mwandishi wetu aliwahi kuwasiliana na ofisi ya Meneja wa Tanroads Mkoa wa Mtwara, lakini alijibiwa kuwa suala la ujenzi na fidia ya wananchi wanaoishi kanda kando ya barabara, ni la kitaifa.

Ofisi hiyo ilimtaka mwandishi aende akaulize makao makuu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Wakati hayo yakiendelea, vikongwe hao na baadhi ya wananchi wanaodai kutolipwa fidia ya nyumba na mali zao nyingine, wametishia kwenda kumuona Waziri Mkuu, ili wamweleze kwa kina madai yao.

Wamedai kuwa safari yao kutoka Nanyumbu kwenda Ruangwa kwenye Ofisi ya Mbunge (Majaliwa), itawahusisha pia wataungana na vikongwe hao.

Wengine watakaoambatana nao ni Eleza Omari na Jafari Machomela Visa.

Uamuzi huo umetangazwa na mtoto wa vikongwe hao, Stambuli Mmole ambaye alisema umekuja baada ya kuona kuwa serikali ngazi ya wilaya na mkoa, zimeshindwa kutatua jambo hilo.

"Ni uamuzi wao wenyewe, wanasema kwa hatua waliyofikia, wanaamini ni Rais Dk. Samia au Waziri Mkuu pekee ndiyo watakaowasaidia kupata haki yao," alisema.

Stambuli alisema, hatua ya wahanga hao imetokana na yeye kulihangaikia jambo hilo kwa muda mrefu, lakini Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Tanroads Mtwara, wameshindwa kuwasaidia.

Awali, akizungumzia sakata zima la vikongwe hao kutolipwa fidia wanazostahili, Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Namasogo, Ramadhan Hussenius, alisema ni kweli mgogoro huo upo na haelewi kwa nini wasilipwe.

"Nyumba za wakazi hao zipo ndani ya mita 60 zinazopaswa kulipwa kisheria na kwa kweli hadi sasa nina malalamiko ya watu watano. Na suala hili hata Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu analijua vizuri," alisema.



# Wanawake 27,000 wafanyiwa ukatili

**Na Mwandishi Wetu, Bagamoyo**

WANAWAKE 27,673 na wanaume 1,434 wamefanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia katika matukio 41,673 yaliyoripotiwa mwaka jana kote nchini.

Hayo yalisemwa katikati ya wiki hii na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo Cha Sheria na Haki za Binadamu LHRC, Anna Henga, alipokuwa akizungumza katika Kongamano la Wajasiriamali lililofanyika mjini Bagamoyo kuelekea Siku ya Wanawake Duniani inayoadhimishwa leo.

“Wanawake 27,673 na wanaume 1,433 wamefanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia katika matukio 41,673 yaliyoripotiwa mwaka jana. Hata hivyo, kwa bahati mbaya sana, wanaume wengi huwa hawajitokezi kutoa taarifa zao,” alisema Henga.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Mohamed Usinga, alielezea kukerwa kwake na matatizo yanayowakumba wanawake katika marejesho ya mikopo.

Alisema wanawake nchini wamekuwa wakmikumbana na changamoto nyingi katika mikopo yanayoipata kupitia taasisi mbalimbali za fedha kiasi cha kuwalazimisha kikumbia nyumba zao.

Mwenyekiti huyo aliwataka wanawake kuelekeza macho ya mikopo katika halmashauri za maeneo yao ambazo alisema sasa zinazotoa mikopo isiyoruhusu unyonyaji na unyanyasaji dhidi ya wakopaji.

“Serikali yetu inayoongozwa na kipenzi chetu Dk. Samia Suluhu Hassan, imeziagiza halmashauri zote nchini zitoe mikopo kwa wanawake, vijana na makundi maalumu, kwa hiyo tumieni fursa hiyo kuondokana na mikopo inayoitwa nyonya damu,” alisema Usinga.

Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Pwani, Hawa Mchafu, aliyeratibu kongamano hilo akishirikiana na kituo hicho, aliwataka wanawake wa Bagamoyo na Mkoa mzima wa Pwani, kuchangamkia fursa ya mikopo ili wajiendeleza kiuchumi.

> **Niipongeze Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kwa kuendelea kutumia asilimia za mapato yake ya ndani kuvikopesha vikundi vilivyoainishwa na serikali ikiwemo vya wsanawake...**

“Niipongeze Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kwa kuendelea kutumia asilimia za mapato yake ya ndani kuvikopesha vikundi vilivyoainishwa na serikali ikiwemo vya wsanawake, vijana na makundi maalum, tuchangamkie fursa hii,” alisema Mchafu.

Naye Mbunge wa Bagamoyo, Muharami Mkenge, aliwaasa wanawake kuwalea watoto ili kuondokana na tatizo la mmomonyoko wa maadili ukiwemo ubakaji.

“Nakumbuka wakati nikiwa mdogo, kulikuwa na muda maalum wa kurudi nyumbani na kulikuwa muda wa kuoga, lakini sasa hivi utakutana na mtoto mpaka saa tano usiku yupo mtaani,” alisema Mkenge.

# CCM Mbeya yaahidi kusafisha propaganda chafu za wapinzani

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephen Mwakajumilo, amewatuliza wakazi wa Mkoa wa Mbeya hususan Jiji la Mbeya akisema Chama kipo imara kuzisafisha propaganda chafu za vyama vya upinzani.

Dk. Mwakajulimo aliyasema hayo alipozungumza na gazeti hili la Mwelekeo kuhusu yaliyojiri kwenye mikutano ya Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) iliyofanyika hivi karibuni.

Katika mikutano hiyo, aliyewahi kuwa Mbunge wa Mbeya Mjini kupitia Chadema, Joseph Mbilinyi, anadaiwa kumtishia Mbunge wa sasa wa jimbo hilo ambaye pia ni Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson.

Dk. Mwakajulimo amesema Wana-CCM hawana hofu wala wasiwasi kuhusu kauli za upinzani kwani wanatafuta



mbinu mbalimbali za kuisambaratisha serikali iliyopo madarakani.

Alisema kwa bahati nzuri CCM na wananchi wanawafahamu vizuri wapinzani kwani wanaishi chini ya uongozi mzuri wa Serikali ya CCM.

Aliwataka wapinzani wa vyama vyote kutambua wazi kwamba CCM ni Chama ambacho kipo madarakani kwa mafanikio makubwa tangu Uhuru wa nchi na kwamba iliruhusu mfumo wa vyama vingi ni kuleta utengamano wa kisiasa ndani ya nchi. “CCM inatambua kwamba malengo ya vyama vya upinzani vinatumia kila aina ya propaganda ili kupotosha wananchi jambo ambalo CCM inalifahamu fika, alisema Dk. Mwakajumilo ambaye ni mchumi.

Alisema CCM inajibu kwa vitendo mkoani Mbeya kwani katika kipindi cha miezi mitatu hadi sasa, zaidi ya miradi mitano mikubwa imesainiwa kuanza kufanyiwa kazi. Aliitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni pamoja na ujenzi wa barabara ya lami kilomita 32 kutoka Ibanda hadi Kajunjumele kwenye Bandari ya Itungi wilayani Kyela. Miradi mingine ni kuleta maji Mbeya kutoka Mto Kiwira wilayani Rungwe, ujenzi wa barabara ya njia nne kutoka Uyole hadi Uwanja wa Ndege wa Songwe na kwamba pia serikali ipo mbioni kujenga upya barabara kutoka Igawa hadi Tunduma. Dk. Mwakajumilo aliwasihi wana-CCM kutowajibu kwa maneno kuhusu kauli mbovu za wapinzani bali watambue kwamba ni propaganda zenye malengo maalum ya kuwayumbisha wananchi.

“Kinachotakiwa kwa Watanzania ni kutambua kazi za maendeleo zilizofanyika katika sekta za afya, elimu, barabara na umeme vijijini,” alisema.

# Vijana waitiwa mikopo ya coaster, bajaj

**Na Mwandishi Wetu, Chalinze**

HALMASHAURI ya Chalinze Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani, imewataka vijana kujiunga kwenye vikundi na kuvisajili li kurahisisha taratibu za kukopa vyombo vya usafiri vya moto zikiwemo basi ndogo za Coaster.

Wito huo ulitolewa juzi na Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Hassan Mwinyikondo, baada ya kukabidhi pikipiki saba zenye thamani ya Sh. milioni 21 kwa Kikundi cha Kazikazi cha Kijiji cha Mboga, kilichotanguliwa na Kikundi cha Bwilingu ambacho hivi karibuni kilikabidhiwa basi aina ya Coaster.

Alisema halmashauri hiyo ina fedha za kutosha zinazosubiri vijana kujiunga katika vikundi ambavyo watavisajili na hatimaye kupata mikopo ya kuwawezesha kuanzisha viwanda vidogo vidogo, kununua mabasi madogo ya Coaster, Bajaj, Bodaboda na Toyo.

“Mbali ya vijana hawa kuwapatia bodaboda hizi, juzi tumekikabidhi mbuzi 100 kikundi cha kina Mama cha Mkwajuni kijijini hapa, wenye thamani ya Sh. milioni tisa ikiwa ni sehemu ya asilimia kumi ya mapato yetu ya ndani,” alisema Mwinyikondo.

Kwa upande wake, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Msoga, Sheila Hatibu, alisema wamepokea Sh. milioni 183 zilizokwenda katika vikundi mbalimbali.

“Vijana wa Kata ya Msoga, tuitumie fursa hii kwani serikali yetu chini ya Rais wetu, Dk. Samia Suluhu Hassan, akisaidiwa na Mbunge Ridhiwan Kikwete, Diwani Hassan Mwinyikondo, Mkurugenzi Ramadhani Possi na wataalamu wote, wanashirikiana kututumikia wana-Chalinze,” alisema Sheila.

Mmoja wa vijana wa Mboga, Michael George, alisema kikwazo kwao ni kukosekana kwa elimu ya namna ya kuunda vikundi na taratibu za kuwawezesha kupata mikopo hiyo.

“Tunaishukuru sana serikali yetu, tunaona na kusikia namna inavyoyahamasisha makundi mbalimbali kuchukua mikopo ili kuwawezesha wanachama kujikwamua kiuchumi. Sisi vijana wa Mboga tunakwama kwa kukosa elimu,” alisema George.

Haji Nageni, Katibu wa Uhamasishaji wa Chipukizi wilayani hapa, aliwataka maofisa maendeleo kuwahimiza vijana kuchangamkia nafasi hiyo.

Mbaraka Mussa, aliishukuru serikali kwa kuwahamasisha vijana kupata mikopo ya kuwawezesha kuendesha shughuli mbalimbali za kiuchumi.



# Samia asafiri na hawa milenia

**Na Mwandishi Wetu**

DUNIA leo inaadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanawake ambapo pamoja na mambo mengine, watu wanatafakari kwa kina hatua za kimaendeleo zilizofikiwa na kundi hilo.

Hatua hizo zinazotokana na ushiriki wa wanawake katika maendeleo ya nyanja mbalimbali, zinaweza kuwa ama za mwanamke mmoja mmoja au makundi ya wanawake.

Nyanja hizo ni pamoja na uongozi, siasa, elimu, kilimo, biashara na hata utoaji wa huduma za kijamii.

Tanzania kama sehemu ya dunia, ina wanawake waliopiga hatua kubwa katika nyanja hizo kiasi cha kuwa watu wa mfano wa kuigwa ndani na nje ya nchi.

Kwa hatua walizopiga, wanawake hao sasa wamekuwa kielelezo cha wanawake wote wa Tanzania kwamba kundi hilo si la watu wa kubezwa kama ilivyokuwa imezoeleka katika karne zilizopita na leo katika gazeti hili, tutaangalia namna baadhi yao tu walivyodhihirisha ukweli huo.

Hawa tunaowaangazia humu leo ni baadhi tu ya wanaoshikilia nyadhifa mbalimbali ndani na nje ya Serikali ya Tanzania na namna utendaji wao unavyowakosha wananchi.

Tunaanza na Mkuu wa nchi, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye takribani miezi miwili iliyopita, Taasisi ya The Royal Al Al-Bayat Institute for Islamic Thought (RABIIT), ilimtaja kuwa miongoni mwa watu wenye ushawishi mkubwa duniani.

Dk. Samia alishika nafasi ya 38 katika orodha ya watu 500 wenye ushawishi mkubwa zaidi duniani. Orodha hiyo ilitolewa na RABIIT mwishoni mwa Desemba, mwaka jana.

Kiongozi huyo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chma Cha Mapinduzi (CCM), alikuwa mbele ya mshambuliaji wa klabu ya Liverpool na Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah.

Dk. Samia ambaye Machi 19, mwaka huu, atatimiza rasmi miaka miwili tangu alipoingia madarakani Machi 19, mwaka 2021, pia amewahi kutajwa na kwa miaka miwili mfululizo, kuwa miongoni mwa wanawake 100 wenye ushawishi zaidi duniani. Alitajwa na Jarida maarufu la Kimataifa la Forbes.

Hali kadhalika ushawishi wake, umempa nafasi ya kuongoza ujumbe wa pamoja wa Afrika katika Kongamano la Kimataifa la Jukwaa la Biashara na Uchumi, lililofanyika Davos, Uswiss mwishoni mwa Januari, mwaka huu.

Lakini pia kati ya Novemba 2 na 4, mwaka mwaka jana, mwanasiasa huyo alizuru China kwa mwaliko wa Rais Xi Jinping na alikuwa wa kiongozi wa kwanza kutoka Afrika kukutana na Xi Jinping tangu achaguliwe tena na Mkutano Mkuu wa 20 wa Chama cha Kikomunisti cha China kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho kwa muhula wa tatu.

Katika ziara hiyo, Dk. Samia alishuhudia utiaji saini wa mikataba na hati 15 za makubaliano ya kimkakati.

Mikataba hiyo iliyolenga kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na uwekezaji kati ya nchi hizo mbili, ni pamoja na ule uliohusu China kuipunguzia Tanzania sehemu ya deni lake la thamani ya Sh. bilioni 31.4.

Mikataba mingine ya kimkakati ni ile inayohusu kuwepo kwa soko kubwa la usafirishaji wa maparachichi na samaki kutoka Tanzania kwenda China.

Pamoja na kuzungumza na mwenyeji wake, Rais Dk. Samia pia alizungumza na Waziri Mkuu wa China na Spika wa Bunge la nchi hiyo.

Rais Samia pia alifanya ziara nyingine nchini Misri ambako alikutana na Rais wa nchi hiyo, Abdel Fattah El-Sisi katika mji wa Sharm El Sheikh.

Viongozi hao walizungumzia ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere unaojengwa na wakandarasi kutoka Misri.

Hii inadhihirisha kuwa mwanamke huyo wa shoka hatajwi kwa upendeleo, bali kwa haki kutokana na namna anavyoyaweka kwenye vitendo yale anayoyawaza na kuyasema.

Kwa hapa nchini, utendaji wake unambeba kwa kila namna na hasa anavyotekeleza miradi ya kiuchumi ya kimkakati ndani ya nchi, huduma muhimu za kijamii, anavyoiweka taswira ya Tanzania katika ramani ya diplomasia na moyo wa maridhiano.

> **Katika utekelezaji wa shughuli hizo, Rais amekuwa akifanya kwa kusaidiwa na mawaziri wa sekta mbalimbali wakiwemo wanawake tisa aliowaamini...**

Mambo hayo na mengine yanayoinufaisha Tanzania na watu wake, yanaongeza ushawishi wake si tu miongoni mwa wananchi, lakini pia kwa viongozi wa nchi za nje na taasisi za kimataifa.

Hii leo, Dk. Samia ni mgeni rasmi katika kilele cha Siku ya Wanawake Duniani akihudhuria sherehe zilizoandaliwa na Baraza la Wanawake la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Bawacha).

Wadadisi wa masuala ya siasa wanatabiri kuwa hatua hiyo inaweza kumpandisha chati katika Uchaguzi Mkuu ujao hasa ikizingatiwa kwamba bado hakuna kada wa upinzani mwenye ushawishi wa kushindana na mgombea wa CCM katika ngazi ya Urais.

Moyo wa maridhiano, usawa wa kijinsia, haki na ustahimilivu wa kisiasa, ni maeneo yanayompa Dk. Samia nafasi ya kuaminiwa zaidi ndani na nje ya Afrika, jambo lilalojenga taswira njema ya bara hili huko 'duniani'.

Hiyo ni sehemu ndogo tu, lakini umuhimu mkubwa kuhusu utendaji wa Rais Dk. Samia ambaye chini ya uongozi wake unaonekana katika namna serikali inavyotekeleza kwa viwango vikubwa miradi mbalimbali kama ilivyoanishwa na Ilani ya CCM.

Katika utekelezaji wa shughuli hizo, Rais amekuwa akifanya kwa kusaidiwa na mawaziri wa sekta mbalimbali wakiwemo wanawake tisa aliowaamini.

Mawaziri hao tisa na...... manaibu si tu kwamba ni wachapakazi, lakini idadi yao ni sehemu ya mkakati wa Dk Samia kuhakikisha kuwa Tanzania inafikia Malengo la Milenia ya idadi sawa ya wanawake na wanaume katika uongozi.

Kwa sasa baraza la mawaziri lina jumla ya mawaziri 25, tisa miongoni mwao ni wanawake.

Wanawake hao kila mmoja katika nafasi yake, wanachapa kazi kubwa inayomvutia si Rais pekee yake, lakini pia wananchi wanaopata huduma za wizara husika.

Lakini wakati Dk Samia akiongoza serikali, Mhimili wa Bunge kwa upande mwingine unaongozwa na mwanamke wa shoka Dk. Tulia Ackson, ambaye pia Mbunge wa Mbeya Mjini (CCM).

Kwa lugha rahisi unaweza kusema kwamba sheria, mipango na bajeti ya nchi kuhusu leo na kesho ya Watanzania iko mikononi mwa mwanamama Dk. Tulia.

Hali kadhalika kuna Dk Stergomena Tax. Huyu ndiye kioo na mwanadiplomasia mwandamizi wa Dk. Samia nje ya mipaka ya Tanzania. Ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, wizara ambayo amewahi kuhudumu kama Katibu Mkuu kabla ya kwenda kuitumikia Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Kabla ya wadhifa wake wa sasa, Dk. Tax alikuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, akiwa mwanamke wa kwanza nchini kushika wadhifa huo.

Miongoni mwao ni pamoja na Ummy Mwalimu, anayesimamia Wizara ya Afya, inayoshughulikia kinga na tiba za wananchi.

Hii ni moja miongoni mwa sekta iliyomwinua Rais Samia na kutajwa na Jarida la Forbes kwa namna alivyoshughulikia janga la UVIKO-19.

Uhamasishaji wake katika chanjo ya ugonjwa huo, ni miongoni mwa vigezo vilivyomfanya aingie kwenye orodha ya Forbes.

Ummy ni Waziri wa Afya ambaye alihangaika mno kushughulikia kwa kiwango cha juu maambukizi ya UVIKO wakati ulipoibuka kwa mara ya kwanza mwaka 2019 .

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaongozwa na mwanamama, Dk. Angeline Mabula, anayesimamia vyema kile anachoelekezwa na bosi wake, Dk. Samia kuanzia sekta ya makazi na upimaji ardhi unavyoendelea nchini.

Kwa mfano, hivi karibuni alishughulikia kwa haraka upimaji wa vijiji katika Bonde la Mto Rufiji, ili kupata maeneo ya uwekezaji mkubwa na wa kisasa katika sekta ya kilimo.

Tayari maeneo ya vijiji 826 vya bonde hilo, vimeshapimwa ndani ya miezi miwili tangu Rais alipotoa agizo la kupima Desemba 22, mwaka jana.

Mama mwingine wa shoka ni Dk. Dorothy Gwajima, anayesimamia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Dk. Dorothy anajulikana kwa namna ya kipekee anavyopambana na ukatili katika jamii. Ni miongoni mwa mawaziri wanaotumia vyema mitandao ya kijamii, kupokea taarifa na kukemea ukatili katika jamii. Ukurasa wake hasa wa Instagram, umekuwa ukiripoti matukio ya ukatili na ameutumia vema kukemea.

Inaendelea uk.5



**Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, baada ya kuwasili kwenye uwanja wa ndege wa Tanga kwa ajili ya kikao na Mawaziri wa Kisekta, Wakuu wa Mikoa ya Tanga na Arusha, Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Tanga, Watumishi, Viongozi wa Kimila na wawakilishi wa wananchi wa Kijiji cha Msomera, Tanga jana. (Picha: Ofisi ya Waziri Mkuu.).**

# Watoto wanaofanyiwa upasuaji moyo `wamwagiwa' misaada

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani, wafanyakazi wanawake kutoka Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), wametoa mahitaji mbalimbali kwa watoto wanaopatiwa matibabu ya moyo kwenye Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) jijini Dar es Salaam.

Kadhalika, wanawake hao wamegharimia matibabu ya upasuaji wa moyo kwa watoto watatu wenye uhitaji waliolazwa katika taasisi hiyo.

"Sisi kama wanawake wa WCF, tunajua ukimsaidia mama umesaidia familia nzima, tunaungana na wanawake wote duniani katika kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani na tunaungana na Rais wetu, Mhe. Dk. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha tunaisaidia jamii nzima," alisema Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano WCF, Laura Kunenge.

Alisema msaada huo mdogo ni ishara kuwa WCF inaunga mkono juhudi zinazofanywa na wataalamu wa taasisi hiyo katika kufanya juhudi za kitabibu, lakini wanapopata usaidizi wa mahitaji mbalimbali kutoka kwa jamii kama ambavyo wao wamefanya inaongeza faraja kwa wagonjwa.

"Tunawaombea watoto wetu wapone upesi na wapate nafuu ya haraka." alisema Kunenge.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Mkurugenzi wa Huduma za Uuguzi JKCI, Robert Mallya, alisema JKCI inapokea wagonjwa wenye uwezo tofauti, kitendo cha wanawake wa WCF kutoa msaada huo wa hali na mali, ni faraja kubwa.

"Tunawashukuru sana kwa msaada waliotoa, wamekuja na mahitaji mbalimbali kama tunavyoona, lakini pia wametoa mchango wa fedha kuhakikisha wale wagonjwa ambao wamekuwa na changamoto ya kukidhi gharama za matibabu, wanaweza kufanya hivyo, tunashukuru sana," alisema Mallya.

Baadhi ya kinamama wanaouguza watoto wao hospitalini hapo, wamewashukuru wanawake wenzao kutoka WCF kwa msaada huo wa mahitaji mbalimbali waliopokea.

"Mimi waliniambia mwanao ana tatizo la valves, kwa hiyo anahitaji kufanyiwa upasuaji, nikasumbuka kutafuta pesa bila mafanikio, lakini nikaambiwa nisubiri, kwa msaada huu, nawashukuru sana," alisema Warda Issa, aliyetokea mkoani Pwani ambaye mwanawe Abdulrasul Jumanne (12), anasubiri kufanyiwa upasuaji wa moyo.



**Mwenyekiti wa Wanawake Tawi la Tughe, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Susan Reuben (kushoto), akimpa mkono mtoto Abdulrasul Jumanne (12), anayesubiri kufanyiwa upasuaji wa moyo katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. WCF imetoa misaada ya mahitaji mbalimbali na fedha za kugharimia upasuaji wa moyo kwa watoto watatu wenye uhitaji wanaopatiwa matibabu katika taasisi hiyo. Msaada huo ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani inayofanyika leo. Wanaoshuhudia ni Dk. Sulende Kubhoja, Mkuu wa Magonjwa ya Moyo kwa Watoto JKCI. (Picha: Mpigapicha Wetu).**

# Samia asafiri na hawa milenia

**Inatoka Uk.4**

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, inaongozwa na Dk. Ashatu Kijaji, ambaye kwa namna ya kipekee, anasimamia utekelezaji wa kazi kubwa inayofanywa na Rais Samia katika kuvutia uwekezaji nchini.

Dk. Pindi Chana, yeye anasimamia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Kwa kifupi, sekta ya burudani inasimamiwa na mwanamke. Sote tunaona Rais Samia anavyohamasisha wachezaji wa klabu za Tanzania zinazoshiriki mashindano ya kimataifa kwa kununua kila goli la kimataifa kwa Sh. 5,000,000.

Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ni Angelah Kairuki, ambaye anasimamia sera na shughuli za serikali katika ngazi za mikoa na wilaya.

Anasimamia pia shule za msingi na sekondari pamoja na walimu. Kwa lugha nyingine ni sawa na kusema kwamba ndiye anayeandaa kina Dk. Samia wajao na wanawake wengine watakaokuwa na dhamana ya walimu na shule za msingi.

Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, nayo iko mikononi mwa mwanamke, Jenista Mhagama.

Hii ni wizara inayosimamia rasilimali watu katika kuhakikisha kuwa watumishi wanawajibika kwa kuzingatia uzalendo, uadilifu na ubora.

Mwingine ni Profesa Joyce Ndalichako, anayesimamia Wizara ya Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, iliyoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Takwimu za sensa ya watu na makazi iliyotolewa mwishoni mwa mwaka jana, zinaonyesha kwamba asilimia 34.9 ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35. Kundi hili kubwa linajumuisha vijana walio katika elimu ya sekondari, vyuo, ajira na biashara mbalimbali.

Wizara hii inawafikia vijana wasio na ujuzi au wenye ujuzi usio rasmi na kuwapa fursa za kuwaingiza katika vyuo vya ufundi ili waweze kulitumikia taifa kwa ajira zenye staha. Wanawake wengine wanaoangaziwa humu leo ni pamoja na, Dk Anna Makakala, Kamishna Jenerali wa Idara ya Uhamiaji aliyeanza kutumikia nafasi hiyo Februari 12, mwaka 2017.

Wakati akitoa sababu zilimzovutia na kumteua Makakala, Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, alisema ni uaminifu wa wanawake wengi katika masuala ya fedha.

Wachambuzi wanamuona Dk. Makakala kama mtu anayeitendea haki na heshima, dhamana aliyopewa kwa sababu kazi anayoifanya katika Idara ya Uhamiaji inaonekana wazi.

Katika Bunge, Rais Dk. Samia naye akamteua Nenelwa Mwihambi kuwa Katibu wa Bunge la Tanzania, akimsaidia Spika Dk. Tulia Ackson.

Mwihambi naye ndiye mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo tangu taifa lilipopata Uhuru wake 1961.

# `Serikali yajivunia Chuo cha Mahakama Lushoto'

**Lusajo Mwakabuku Na Felix Chakila**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, amesema Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) ni cha mfano wa kuigwa katika utoaji wa mafunzo elekezi ya awali na endelevu ya kimahakama.

Dk. Ndumbaro aliyasema hayo juzi alipotembelea chuo hicho na kuzungumza na uongozi, menejimenti ya watumishi na wafanyakazi wa IJA.

"Wizara ya Katiba na Sheria, inajivunia kwa uwepo wa chuo hicho ambacho kimebeba taswira ya nchi husussan kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo kimeendelea kuwa mfano wa kuigwa kama chuo kinachojenga na kuimarisha kada ya sheria," alisema Dk. Ndumbaro.

Alisema chuo hicho ni kitovu na kisima cha elimu bora.

"Kimsingi, chuo kina uwezo wa kujenga taaluma na kuwanoa wataalam mbalimbali wa sheria wanaokwenda kusimamia haki wakiwemo mahakimu na watumishi wengine wa mahakama," aliongeza Dk. Ndumbaro.

Akizungumza baada ya kukagua mazingira ya chuoni hapo yakiwemo mabweni, Dk. Ndumbaro alibainisha kuwa chuo hicho kimekuwa kikifanya kazi nzuri kwa kutoa mafunzo mbalimbali elekezi na endelevu kwa watumishi wa Mahakama ya Tanzania.

Alisema lengo la kutoa mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa kutenda haki kwa wote na kwa wakati kwa kuzingatia misingi ya sheria na uadilifu.

# Vijana watakiwa kuzitumia maskani kuboresha uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili Muungano na Mazingira, Khamis Hamza Chilo, amewataka vijana kuzitumia maskani kujifunza vitu mbalimbali vitakavyowasaidia kuongeza kipato chao cha kila siku na kuacha kuwa tegemezi.

Akizungumza na vijana hao baada ya kukabidhi runinga kwa vijana wa Maskani ya Bekari iliyopo Mpapa Wilaya ya Kati Unguja, Naibu Waziri alisema umefika wakati kwa vijana kuzitumia maskani kuboresha hali zao za kiuchumi.

Aidha, aliwaonya vijana hao kuacha kuonesha michezo itakayohamasisha kujiingiza katika vitendo viovu ikiwa ni pamoja na matumizi ya dawa za kulevya, ujambazi na vingine visivyofaa katika jamii.

Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, Haji Shaaban Waziri, kwa upande wake, aliwaasa vijana hao kukemea na kutoa elimu ya kupinga vitendo vya udhalilishaji.

Alisema kwa sasa Zanzibar inakabiliwa na janga la udhalilishaji huku takwimu zikionesha asilimia kubwa ya wafanyaji wa vitendo

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO



### Bodaboda kutotii Sheria za Barabarani

**SASA imekuwa kama ni kawaida kwa waendesha pikipiki maarufu kama `bodaboda' kutozingatia Sheria za Barabarani na hivyo kuwa moja ya vyanzo vya ajali katika maeneo mengi ya miji na majiji. Ni jambo la kusikitisha kuwaona waendesha bodaboda wengi, wakipuuza kabisa sheria hizo kana kwamba wao wako juu ya sheria. Kwenye alama za pundamilia (zebra crossing), wao hupita tu tena kwa kasi pasipo kujali kama ni maeneo ya vivuko kwa waenda kwa miguu, lakini hawajali hata kama taa nyekundu zitaashiria wasimame. Jirekebisheni na zingatieni sheria bila shuruti.**



## MAONI YA MHARIRI

# Wanawake wamethibitisha kuwa wanaweza

LEO Machi 8, ni Siku ya Wanawake Duniani. Ni siku ambayo wanawake wote katika nchi mbalimbali duniani, huiadhimisha na kuitukuza kama siku yao maalum na inatambuliwa na Umoja wa Mataifa (UN).

Chanzo cha Siku ya Wanawake Duniani ni mwaka 1908 baada ya wanawake 15,000 katika Jiji la New York, Marekani kuandamana wakidai muda mfupi wa kufanya kazi, malipo bora na haki ya kupiga kura.

Mwaka mmoja baadaye yaani 1909, Chama cha Kisoshalisti cha Marekani, kilitangaza Siku ya Kitaifa ya Wanawake ya kwanza.

Wazo la kuifanya siku hiyo kuwa ya kimataifa, lilitoka kwa mwanamke mwanaharakati wa kikomunisti na mtetezi wa haki za wanawake, Clara Zetkin.

Mwanaharakati huyu wa Kikomunisti, alipendekeza wazo hilo mwaka 1910 katika Mkutano wa Kimataifa wa Wanawake waliokuwa wakifanya kazi huko Copenhagen.

Kulikuwa na wanawake 100 huko kutoka nchi 17, na walikubali pendekezo lake kwa kauli moja.

Kwa mara ya kwanza, iliadhimishwa mwaka 1911 Austria, Denmark, Ujerumani na Uswizi na mambo yaliwekwa rasmi mwaka 1975 wakati UN ilipoanza kuadhimisha siku hiyo.

Miaka 100 iliadhimishwa mwaka 2011, kwa hiyo, mwaka huu, tunasherehekea siku ya 123 ya Kimataifa ya Wanawake.

Wanawake nchini Tanzania kama ilivyo kwa wenzao katika nchi nyingine duniani, pia huadhimisha siku hii.

Na kwa kutambua mchango wao mkubwa kwa taifa hili, hivi sasa wanawake wengi wapo katika nafasi nyingi za uongozi.

Mathalani, Kiongozi Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni mwanamama.

Aidha, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni Dk. Tulia Ackson, ambaye pia ni mwanamama.

Si hao tu, wapo mawaziri na naibu mawaziri wanawake ambao utendaji na uwajibikaji wao, ni dhahiri umethibitika mbele ya wananchi.

Tukiangalia utendaji wa Rais Samia ndani na nje ya nchi hasa anavyoipeperusha Bendera ya Tanzania na Afrika katika anga la kimataifa tunaona fahari kubwa.

Tunaona utendaji unaoacha alama kwa vizazi vingi kwa namna anavyotekeleza miradi ya kimkakati ya maendeleo, demokrasia na usawa wa kijinsia.

Hakika wanawake wanaweza si tu mpaka wawezeshwe, endeleeni kujiamini jamii inawaamini.


## UMGL MEDIA Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255693257410 / 0766005061
**Mhariri Michezo:** +255713055011 / 0621350860
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** jaridalamwekeleo@gmail.com




Na Prosper Mhadisa
JICHO LANGU
jaridamwelekeo@gmail.com

# Vijana zingatieni tabia njema, hekima

"UZURI si sura, pozi na maumbile kama wengi wanavyodhani, uzuri ni tabia, hekima na ukarimu wako, busara na imani." Ni moja ya mistari ya kibao cha muziki "Nikikupata" cha Benard Paul, almaarufu kama Ben Pol.

Tuachane na nikikupata, halafu tuingie katika maana nyingine ya kimaisha tukitumia kipande hicho kizuri sana kutoka kwa msanii huyo.

Jamii ya sasa ni jamii iliyopiga hatua kubwa ya kimaendeleo katika nyanja mbalimbali na hasa za kiuchumi na kisiasa. Maendeleo makubwa sana yamefikiwa kupitia nyanja hizi. Lakini ili kufikia maendeleo hayo, watu walipitia njia na hatua mbalimbal. Hata hivyo, kubwa kuliko zote ni tabia, hekima, ukarimu, busara na imani ndani ya ufanyaji shughuli mbalimbali.

Kama sehemu ya jamii, tunapaswa kutambua na kutilia maanani suala la tabia njema kila mahali.

Hii inajumuisha mahali pa kazi, nyumbani, kijiweni wakati ukipiga stori na rafiki zako na sehemu nyingine yoyote yenye mikusanyiko ya watu.

Mazingira haya yanaweza kumlinda mtu katika mema kutokana na tabia nzuri atakayoionesha na ndiyo maana katika kibao hicho cha Nikikupata, Ben Pol anasisitiza umuhimu wa uzuri wa tabia njema katika maisha.

Katika hali ya kawaida, ni rahisi sana kwa mtu mwenye tabia nzuri kufanikiwa kimaslahi na kiafya kwa sababu ya uhusiano wake mzuri na jamii ya watu wanaomzunguka hususani waliofanikiwa kwa kuzingatia kuwa wao, wanapenda sana kuwa karibu na wale wenye tabia nzuri. Lakini pia jamii inapaswa kuwa na watu wenye hekima na busara katika kila hatua inayopigwa. Hekima na busara zinazozungumziwa hapa ni katika matumizi ya lugha, hekima na ustadi wa kufanya jambo.

Siku hizi, watu wengi hasa vijana, wamekumbwa na tatizo la kukosa hekima na busara katika matumizi ya lugha na hivyo kusababisha kukosa ustadi wa kufanya mambo.

Wamekuwa wakitumia lugha zisizofaa katika mazingira yasiyostahiki kutumika. Wanatumia lugha za matusi, kejeli, dharau au kumdhihaki mtu bila ya kujali ni mtu wa aina gani na ni katika mazingira yapi.

> **Mazingira haya yanaweza kumlinda mtu katika mema kutokana na tabia nzuri atakayoionesha na ndiyo maana katika kibao hicho....**

Mbaya zaidi wanatumia lugha hizo hata katika mazingira ya ofisi, kitendo ambacho kinaweza kusababisha mtu kukosa kazi kwa kushindwa kuyaelewa mazingira. Lugha za namna hiyo zimekuwa zikitumika pia katika maeneo yenye umati wakiwemo wazee na matokeo yake ni, wazee kushindwa kutoa maarifa yao kwa vijana wanaochipukia.

Wengi wao hupenda kuwatukana wazee, kuwadharau na kuwakejeli kwa madai kuwa umri wao umepita. Hii si sahihi hata kidogo kwa sababu maarifa ya kizazi cha wazee ni muhimu sana.

Kwa msingi huo, napenda kuishauri jamii kwamba, hakuna mafanikio yanayoweza kuja bila jamii ya watu kuwa na tabia njema, hekima, ukarimu, busara na imani.

Ili ufanikiwe ni lazima uwe na tabia ya unyenyekevu, hekima katika matumizi ya lugha na imani kwa watu

# Posta Afrika yajipanga kuongeza wanachama

**Na Claud Gwandu, Arusha**

UMOJA wa Posta Barani Afrika (PAPU), umepanga kuongeza idadi ya nchi wanachama wake ili kuwezesha huduma hizo muhimu kufikia wananchi wengi zaidi barani humo.

Moja ya mikakati ya kuongeza wanachama hao, ni kushawishi nchi ambazo bado hazijawa wanachama, kujiunga na umoja huo kwa kutumia ofisi za kidiplomasia za nchi hizo zilizopo hapa nchini. Katibu Mkuu wa Umoja huo, Sifundo Chief Moyo, alisema mjini hapa hivi karibuni kuwa mkakati uliopo ni wa kuzishawishi nchi nyingine 10 za Kiafrika ambazo si wanachama kujiunga na PAPU.

"Nguvu yetu kama umoja ni mshikamano wetu uliopo na kuwaongeza wenzetu katika umoja huu muhimu kwa maendeleo ya huduma za Posta katika karne hii ya mawasiliano na tutawafikia ili tuwashawishi waone umuhimu wa kuwa wanachama.

"Tutatumia njia za kidiplomasia hasa kwa kuwafikia wawakilishi wa nchi hizo waliopo Tanzania na tuna matumaini makubwa kwamba mkakati huo utafanikiwa,"alisisitiza Moyo na kuongeza:

"PAPU ni ya Waafrika wote lakini kuna nchi kama kumi hivi ambazo bado hazijawa wanachama hivyo ni wajibu wangu kuzishawishi wajiunge nasi na tutajadiliana na wawakilishi wa nchi hizo waliopo Tanzania ili nao wawe wanachama," alisema.

**Tutatumia njia za kidiplomasia hasa kwa kuwafikia wawakilishi wa nchi hizo...**

Dk. Moyo alikuwa akizungumza katika ziara ya wawakilishi 14 wa nchi za Kiafrika (ADG) waliopo nchini waliojionea maendeleo ya ujenzi wa jengo la kisasa la makao makuu ya PAPU jijini hapa.

Ujenzi wa jengo hilko upo katika hatua za mwisho za kukamilika.

Jengo hilo lenye urefu a ghorofa 17, linajengwa kwa ushirikiano wa PAPU na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na linatarajiwa kukamilika baadaye mwezi huu. Kukamilika na kuanza kutimika kwa jengo hilo, kutafufua na kuchochea utoaji wa huduma za Posta barani Afrika kwa kuzingatia maendeleo ya teknolojia ya hivi sasa.

Alitaja nchi zinazolengwa katika mkakati huo kuwa wanachama wa umoja huo kuwa ni pamoja na Cape Verde, Djibout, Guinea Bissau, Mauritius, Mauritania na Rwanda.

Nyingine ni Sudan Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kiislamu ya Sahara, Sao Tome na Principe na Seychelles ambazo bado si wanachama wa PAPU.

Kwa mujibu wa Dk. Moyo, kwa mwaka huu wa fedha nchi wanachama zimelipa asilimia 47 tu ya kiasi cha dola za Marekani milioni 1.4 wakati kiasi cha madeni wanayodaiwa nchi wanachama kimefikia dola za kimarekani milioni 6.3 hadi ilipofikia Februari 20,mwaka huu. Akizungumza kwa niaba ya wawakilishi hao, Balozi wa Burundi nchini Tanzania, Gervais Abayeho, alipongeza jitihada za Umoja huo za kuendeleza huduma za Posta barani Afrika, hasa katika kipindi hiki cha maendeleo makubwa ya kiteknolojia duniani. "Tumevutiwa sana na kuridhika na jitihada mnazoendelea kufanya katika kuimarisha huduma za Posta barani Afrika na ujenzi wa jengo hili ni mfano dhahiri wa kuthibitisha jitihada zenu na tutashirikiana kuimarisha huduma hizo katika bara letu," alisema Balozi Abayeho.

Umoja huo ulioanzishwa Januari 18, 1980 jijini Arusha, ulitarajiwa kuimarisha huduma za Posta na kuwa sehemu muhimu ya kuimarisha uchumi wa kidijiti barani Afrika.

Kukamilika kwa makao makuu hayo ambayo yatakuwa makao ya Sekretarieti ya umoja huo,yatasaidia kuongeza kasi ya kuimarisha huduma za Posta kidigitali barani Afrika.

# ZRA sasa yajitosa shuleni kutoa elimu ya ulipaji kodi

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mapato Zanzibar (ZRA), imeanzisha klabu za skuli za sekondari Unguja na Pemba kwa lengo la kutayarisha walipakodi wa baadaye na kuhakikisha zinachagiza ulipaji kodi wa hiari.

Ofisa Elimu ya Kodi kutoka ZRA, Raya Suleiman Abdallah, alieleza hayo mara baada ya kuzungumza na wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha tatu katika Shule ya Sekondari Kidoti Mkoa wa Kaskazini Unguja ikiwa ni mwendelezo wa mamlaka hiyo kutoa elimu ya kodi kwa wanafunzi wa shule za sekondari za Zanzibar.

Alisema ZRA imeamua kuanzisha klabu hizo kwa kuteua shule 22 zikiwemo 14 Unguja na nane Kisiwani Pemba.

Alizitaka shule hizo kwa Unguja ni Benbella, Haile Selassie, Dk. Salmin Amour Juma, Trifonia Academy, Zanzibar Commercial, Kidoti, Donge, Nungwi, Fujoni, Makunduchi, Hasnuu Makame, Bambi, Umoja Uzini na Mikindani Dole. Kwa Pemba ni Fidai Castro, Shamiani, Chambani, Mizingani, Chasasa, Mbuzini, Tumbe na Skuli ya Sekondari Wingwi.

Raya alifafanua kuwa katika klabu hizo, kutakuwa na mashindano ambayo yataanza ngazi ya wilaya, mkoa hadi ngazi ya taifa ili kuhakikisha kwamba wanaipata vizuri taaluma ya kodi. Aliwaomba wanafunzi kushirikiana na mamlaka hiyo katika kuisaidia serikali kupata mapato yake hasa kuchagiza ulipaji kodi wa hiari. "Wanafunzi wanawajibu mkubwa wa kuisaidia serikali pale wanapodai risiti wanapofanya manunuzi na pia kutusaidia kuwapa elimu wafanyabiashara kuhakikisha wanasajiliwa na kuwa walipakodi wanaotambulika ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato nchini," alisema.

Naye Asha Ali Hassan, Ofisa Uhusiano wa mamlaka hiyo, alisema changamoto zinazoikabili mamlaka hiyo ni kuwepo kwa wafanyabiashara wanaofanya biashara bila ya kusajiliwa kulipa kodi, kuwepo kwa biashara ya mafuta ya magendo nchini, wanunuzi kutodai risiti wanaponunua bidhaa, wauzaji kutokutoa risiti wanapofanya mauzo na upatikanaji wa taarifa sahihi kwa baadhi ya walipakodi.

Hivyo aliwataka wanafunzi na wananchi kushirikiana katika ukusanyaji na usimamiaji wa mapato ya serikali, kuwa karibu na maofisa wa kodi kwa lengo la kupata elimu na ufafanuzi wa changamoto mbalimbali zinazojitokeza, kufanya biashara na wafanyabiashara wanaofuata sheria. Nao wanafunzi wa skuli hiyo, waliahidi kuwa mabalozi wazuri wa kodi ili kuona nchi yao inaendelea kupiga hatua za kimaendeleo.



**Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, akipanda mti kwenye bustani ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto mkoani Tanga juzi. (Picha: Mpigapicha Wetu).**

# Wanafunzi waomba kulindwa dhidi ya udhalilishwaji

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

WANAFUNZI wa shule ya Memon Academy wamewaomba walimu kuwalinda zaidi wakati wanapokuwa skuli ili kuepuka kukumbwa na vitendo vya udhalilishaji. Wakizungumza mara baada ya kupatiwa elimu kuhusu udhalilishaji wa kijinsia shuleni hapo, wanafunzi hao walisema muda mwingi wanautumia wakiwa skuli, hivyo wahitaji kupata ulinzi zaidi kutoka kwa walimu wao kwani mazingira ya shule nayo yanaweza kuwa hatarishi kwao. Mwanafunzi Abdallah Abdulkadir, wa darasa la sita katika shule hiyo, alisema kutokana na elimu waliyopatiwa, sasa wanafahamu kwamba kuna madhara mengi yanayoweza kuwapata iwapo watakumbwa na udhalilishaji hasa wa kingono na kusababisha kuvunjika ndoto zao za kimaisha. "Sisi watoto tunapopata udhalilishaji, tunaathirika kimwili na kiakili hata kama tuna ufahamu mzuri skuli, lakini tukishapata vitendo hivyo, akili zetu za kusoma zinakuwa siyo nzuri tena," alisema mwanafunzi huyo.

Naye mwanafunzi Ammal Altaf, alisema elimu waliyopatiwa, itawasaidia kujihadhari na vitendo vya udhalilishaji ambavyo vinaweza kuathiri maisha yao.

Wakitoa elimu shuleni hapo, wanamtandao wa kupinga vitendo vya udhalilishaji Mkoa wa Mjini Magharibi, walisema ni vyema wanafunzi wanapopoona viashiria vya kutokea vitendo hivyo kutoa taarifa kwa walimu wao na nyumbani kuwaambia wazazi wao ili hatua zichukuliwe haraka. Mwanamtandao Mariam Juma Simai, aliwataka wanafunzi hao kujenga tabia ya kukataa kupokea vitu mbalimbali wanavyopewa na watu na kutoa taarifa ili kufuatiliwa dhamira ya watoaji.

"Na zaidi sasa watu wanawapa watoto simu za mkononi tena wadogo wa kike, zinatiwa MB, baadaye wanawafungulia ile michezo michafu wanaambiwa waangalie kisha walichokiona humo wanatakiwa wawafanyie wenzao," alisema Mariam.

Kwa upande wake, Mwalimu wa shule hiyo, Is-haka Omar Suleiman, alisema watahakikisha usalama wa wanafunzi wao unaimarika skulini hapo na kuendelea kupatiwa elimu ili kujilinda wakati wote.

Afisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Mjini, Mithle Hussein Mussa, alisema ni vyema watoto kuondoa usiri wanapokutwa na jambo lolote na badala yake watoe taarifa ili iwe rahisi kukabiliana nalo wawe salama. Afisa Msimamizi wa Kitengo cha Masuala ya kupinga udhalilishaji kutoka Chama cha Waandishi wa Habari wanawake Tanzania Tamwa Zanzibar Zaina Salum Abdallah amesema lengo la kutoa elimu hiyo ni kukuza uelewa wa wanafunzi wa skuli ili waweze kukabiliana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

# Jenerali Mabeyo aitaka NCAA kuingiza watalii milioni tano

**Na Lauden Mwambona, Songwe**

VIONGOZI wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), wametakiwa kubuni fursa zaidi za utalii ili ifikapo mwaka 2025, watalii milioni tano wawe wameingia nchini. Agizo hilo limetolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya NCAA, Mkuu wa Majeshi Mstaafu , Jenerali Venance Mabeyo, alipozungumza kwenye uzinduzi wa makumbusho ya Kimondo kilichopo wilayani Mbozi mkoani Songwe mwishoni mwa wiki.

Jenerali Mabeyo alisema kufunguliwa kwa makumbusho ya Kimondo, kunafungua fursa za kiuchumi kwa wananchi wa Songwe na kuwavutia watalii wengi kuja kuangalia mila, tamaduni na desturi pamoja na fursa za uwekezaji.

Alisema makumbusho hayo ya kisasa, ni ya 10 katika taifa na kwamba makumbusho hayo lazima yatumike kikamilifu kuvutia watalii na wawekezaji.

Aliitaka NCAA kujipanga vema kwa kutafuta vivutio vingine na kuhakikisha wanapata watalii milioni tano ifikapo mwaka 2025. Awali , Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Francis Michael, akizungumza kwenye hafla hiyo, pamoja na kuwapongeza NCAA kwa makumbusho, alisema mkoa wake kwa sasa unaanza maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Kimondo yanayofanyika Juni 31, kila mwaka duniani. Alisema siku hiyo ni fursa ya kutangaza vivutio vilivyomo mkoani Songwe vikiwamo vya maji moto mengi zaidi na Kimondo ambacho ni cha pili kwa ukubwa Afrika. Kimondo



cha Mbozi kinakadiriwa kuwa na uzito wa tani 12 wakati kimondo cha nchini Namibia kina uzito wa tani 60 na ndicho kimondo kikubwa zaidi Afrika na duniani. Taarifa za NCAA znaonyesha kuwa Kimondo cha Mbozi kiligunduliwa na Mwafrika aliyejulikana kwa jina la Mzee Halele ambaye alikuwa mhunzi katika harakati zake za kutafuta chuma alikiona kimondo hicho na baadaye kumbukumbu za kimondo hicho ziliwekwa kwenye maandishi na mzungu aliyeitwa Wiliam Nolt, mwaka 1930. NCAA imekiweka Kimondo kwenye hifadhi zake, jambo lililosababisha wakazi wa eneo la karibu na kimondo hicho kuondolewa.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa CCM Mkoa Radwell Mwampashe, ameitaka mamlaka hiyo kuwalipa fidia wananchi hao ili kuondoa manung'uniko. Kufuatia kauli hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya NCAA, Jenerali Mabeyo amewatoa hofu wananchi wa Mbozi akisema Serikali inayoongoizwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ni sikivu na haiwezi kushindwa kuwalipa wananchi Sh. bilioni 1.4.

# Watakiwa kuiunga mkono serikali maboresho huduma za afya

**Na Mwandishi Wetu, Iringa**

WANANCHI wametakiwa kuendelea kushirikiana na kuiunga mkono serikali, katika maboresho ya huduma za afya nchini ili kuhakikisha huduma hiyo inatolewa kwa kiwango cha juu na kwa wakati.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Dk. Godlove Mbwanji, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya na Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Afya katika usimamizi wa miradi ya maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19 kwa Nyanda za Juu Kusini, alipotembelea Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali inayotekelezwa kwa fedha za UVIKO-19.

Dk. Mbwanji alisema wananchi wanapaswa kushirikiana na serikali kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya, ili kuhakikisha kila Mtanzania ana afya nzuri na kushiriki katika ujenzi wa taifa.

"Serikali inafanya kazi kubwa sana kuboresha huduma za afya, nitoe wito kwa mtu mmoja mmoja, wafanyabiashara na taasisi mbalimbali za kifedha kwenye yale maeneo mbalimbali wanaoweza wasaidie, ili kusudi wote tushirikiane kuhakikisha Watanzania tunakuwa na afya nzuri ya kulea tija pia katika kukuza uchumi wa nchi yetu," alisema Dk. Mbwanji.

Aidha, aliupongeza uongozi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa chini ya Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mkoa wa Iringa, Dk. Alfred Mwakalebela, kwa usimamizi mzuri wa fedha za mradi na kuwasihi watumishi kutunza vifaa hivyo na miundombinu hiyo ya kutolea huduma ili idumu kwa muda mrefu.



Pia, Dk. Mwakalebela, aliishukuru serikali kwa kuwapatia Sh. bilioni 3.8 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba ili kutoa huduma kwa wananchi wa Iringa na mikoa ya jirani.

Baadhi ya vifaa tiba hivyo ni CT- Scan na mashine ya Digital X-Ray pamoja na fedha kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa nyumba ya mtumishi, Wodi ya Uangalizi Maalum (ICU), Jengo la Radiolojia na Tiba Mtandao (Telemedicine).

Nao wakazi wa Mkoa wa Iringa, Rehema Daud na Arensto Mwaigaga, kwa nyakati tofauti, waliishukuru serikali kwa uwekezaji mkubwa katika kuendelea kuboresha mazingira ya kutolea hospitalini hapo. Jumla ya Sh. bilioni 3.88, zilipokelewa na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa kwa ajili ya ujenzi/ukarabati majengo ya ICU, Radiolojia, ujenzi wa nyumba ya mtumishi na ununuzi wa vifaa tiba.

# Wanafunzi wapigwa jeki magodoro 60

**Na Abdul Mitumba, RUANGWA**

JAMII ya watu wa Wilaya ya Ruangwa katika Mkoa wa Lindi, imeshauriwa kuongeza kasi ya uwekezaji katika sekta ya elimu kwa watoto hasa wenye mahitaji maalum ili kuwasaidia kufikia malengo ya kujikomboa dhidi ya ujinga na umaskini.

Wito huo ulitolewa hivi karibuni na Diwani wa Kata ya Nachingwea, Mahamoud Sadik, alipokuwa akizungumza katika hafla fupi ya kupokea msaada wa magodoro 60 kutoka kampuni ya uchimbaji madini ya Ngwena Tanzania Limited.

"Kama wadau wa elimu, hii ni siku ya furaha kwa sababumsaada huu umekuja huku serikali ikiwa imekamilisha ujenzi wa bweli kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi Namakonde," alisema.

Sadiki alisema kampuni ya Ngwena inastahili kupongezwa hasa ikizingatiwa kuwa imetoa msaada huo hata kabla haijaanza rasmi uchimbaji wa madini katika mgodi wake wa Nangurugai uliopo Kata ya Mbwemkuru wilayani hapa.

> **Kama wadau wa elimu, hii ni siku ya furaha kwa sababu msaada huu umekuja huku serikali...**

Diwani huyo alisema serikali imejenga mabweni mawili yenye thamani ya Sh. milioni 160, lakini wanafunzi walishindwa kuanza kuyatumia kwa kukosa vifaa yakiwemo magodoro.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Ngwena, Phils Hoskins, alisema msaada huo ni sehemu ya uwajibikaji kwa jamii zenye uhitaji maalum na kwamba wataendelea kufanya hivyo.

Kampuni ya Ngwena ni miongoni mwa kampuni kubwa zilizowekeza katika sekta ya madini wilayani Ruangwa. Nyingine ni Urenex na Lindi Jumbo Tanzania. Akitoa shukrani kwa msaada huo, Mkuu wa shule hiyo, Giles Mohamed, alisema shule yake ina wanafunzi 35 wenye mahitaji maalum.

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Mweleko

JARIDA

# Jungu kuu

Jumatano Machi, 8-14, 2023

UCHUMI | ELIMU | BIASHARA | SIASA

**Jarida hili haliuzwi**



# Ruangwa yavuka lengo ujenzi shule za sekondari kila kata



UK. 11

## Nyerere: Chama ni cha dini zote, makabila yote na koo zote

## Wajue aina tano ya wateja na sifa zao

UK. 16



siasa

# Nyerere: Chama ni cha dini zote, makabila yote na koo zote - 2

**Na Mwandishi Wetu**

**TANU na Raia ni kitabu kilichoandikwa na aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hayati Julius Nyerere. Sehemu ya kwanza ya kitabu hiki, ilianikwa katika toleo lililopita na ifuatayo ni sehemu ya pili na mwisho ya kita**

BINADAMU wanapofanya umoja wa aina yoyote huwa wanayo shabaha ya kuunda umoja huo. Pengine ni umoja wa kujipatia elimu, au wa kufanya biashara, au wa kucheza ngoma, au kuimba nyimbo, au kwenda kumzika jirani, na kadhalika. Vitendo vyao vyote huwa vina shabaha ile moja, yaani kuzidi kuunda umoja huo. Vitendo vyao vizuri ni vile vinavyosaidia kuitimiza shabaha yao na vibaya ni vile ambavyo vinapinga kutimizwa kwa shabaha yao havihusiani kabisa kutimizwa kwa shabaha hiyo.

Sisi tulipounda TANU, tuliipa shabaha moja kubwa; kuondoa serikali ya kikoloni katika nchi yetu. Lakini katika kutimiza shabaha hiyo tulikuwa nazo shabaha nyingine, moja kubwa kati ya hizo ni kule kuunda umoja wenyewe ambao ndiyo chombo cha kutimizia shabaha kuu ya kuondoa serikali ya kikoloni na kuleta serikali yetu wenyewe.

Vitendo vyetu vilivyokuwa vikisaidia kutimiza shabaha yetu ya UHURU wetu na kuinua hali ya maisha ya watu wa nchi yetu. Katika kuvihukumu vitendo vyetu kama ni vizuri, au ni vibaya, hatuna budi tujiulize:

Je, vinasaidia au vinapinga kutimiza shabaha ya Chama chetu? Kama vinasaidia ni vizuri. Kama vinapinga ni vibaya, na yafaa tuviache.

### UONGOZI WA TANU

Tulipokuwa tukiondoa serikali ya kikoloni tulikuwa na shabaha pia ya kuyaondoa maovu yote yaliyoandamana na serikali ya kikoloni. Uongozi katika serikali ya kikoloni ulikuwa hautokani na Raia wa nchi yetu. Viongozi walibandikwa kutoka juu au kwa nguvu tu, au kwa hila au kwa rushwa, na japo hawakupendwa na raia waliendelea kukaa katika uongozi. Jambo hili tuliona ni miongoni mwa maovu ya kikoloni ambayo hayana budi yazikwe pamoja na ukoloni wenyewe.

Uongozi wa kwanza ambao hatuna budi tuhakikishe kuwa unatokana na raia wenyewe ni uongozi wa TANU Kila mmoja wetu aliye katika hali ya uongozi – toka President mpaka Chairman wa kijiji, toka Secretary General mpaka Secretary wa kijiji –hana budi ajiulize; Ikiwa nilichaguliwa kwa kura, hizo kura nilizipataje? Nilizipata kwa hila, kwa rushwa, kwa vitisho, au kwa ujanja wa aina yoyote, au nilizipata kwa hiari ya wapiga kura wenyewe? Ikiwa cheo changu ni cha kuajiriwa, siyo cha kuchaguliwa kwa kura, je kuajiriwa kwangu kulitokana na hila, vitisho, rushwa, au ujanja wa aina nyingine yo yote, au kwa njia safi kabisa?

Asili ya uongozi wetu ni mbili: Ya kwanza ni WATU. Hatukutumwa kutoka katika mwezi kuja kuongoza watu wa nchi hii. Wala sisi si viongozi wa kikoloni kwamba tulitumwa na Serikali ya Kigeni kuja kuongoza watu wa nchi hii. Uongozi wetu hauna budi utokane na watu wa nchi hii, bila rushwa, bila vitisho na bila ujanja wa aina yo yote. Tunapofika katika hali ya uongozi kwa kupitia mlango wa hila au rushwa, au vitisho, au ujanja wa aina nyingine yo yote, basi hatukutokana na watu wenyewe.

Asili ya pili ya uongozi wetu ni HAKI. Tuliunda TANU iondoe ukoloni pamoja na maonevu na dhuluma za aina yo yote zilizo ambatana na ukoloni. Lakini HAKI ni HAKI kwa WATU, siyo kwa majani au miti. Basi, tukifika katika hali yetu ya uongozi kwa njia yo yote ambayo si ya HAKI, ni wazi kwamba haiwezekani kwamba tuwe tumetokana na watu wenyewe. Japo kama uongozi wetu haukutokana na kura za watu, bali ni wa kuajiriwa, ni wazi kuwa tumeufikia kwa njia ya hila, rushwa, vitisho au ujanja wa aina yo yote, hauwezi ukwa uongozi wa HAKI na hauwezi ukawa UONGOZI WA WATU. WATU na HAKI ni misingi ya uongozi ambayo haiachani.

Nikisema hivyo, siyo kwamba kiongozi asiye chaguliwa na WATU hawezi akatenda yaliyo HAKI. Anaweza.

Maana yangu ni kwamba walinzi wa HAKI za WATU ni watu wenyewe.Kutegemea haki zao zilindwe na viongozi wasiotokana nao ni jambo la kubahatisha. Wanaweza wakapata viongozi wazuri, na hiyo itakuwa bahati yao. Lakini wakipata viongozi wabaya watakuwa na

> **Viongozi wa TANU hawana budi watokane na watu kwa sababu TANU ni Chama cha watu...**

bahati mbaya sana, kwa sababu watakuwa hawana dawa ya kuwaondoa.

Kwa sababu Chama chetu ni chama cha watu wa nchi hii, basi viongozi wa TANU hawana budi wachaguliwe na WATUWATU na nchi hii, na kwa njia za wazi wazi na za HAKI.

Viongozi wa TANU hawana budi watokane na watu kwa sababu TANU ni Chama cha watu. Lakini sababu ya pili ni kwamba kazi ya TANU ni kuwatumikia watu. Sitaki kueleza mambo yanayo fanywa na serikali - kama vile kujenga shule, hospitali, barabara na kadhalika.

Nataka kusema juu ya shida za kila siku za watu wetu.Hatuwezi tukawa kweli chama cha watu ikiwa hatujishughulishi na shida za kawaida za watu wetu. Hata kama tukijenga shule za kutosha, hospitali za kutosha, barabara zakutosha, tutakuwa bado hatujawa chama cha watu ikiwa hatujishughulishi na shida na matatizo na furaha zao za kila siku.

Maganga bin Musa aliunguliwa nyumba yake jana. Wakuu wetu wa TANU wamepata habari kwamba nyumba ya Maganga bin Musa iliungua jana. Yawezekana kuwa walisikitika sana walipopata habari hiyo.

Lakini kusikitika peke yake hakutoshi. Shida ya maganga bin Musa na mkewe na watoto wake haitaondolewa kwa masikitiko matupu ya viongozi wa TANU na wanachama wake. Shida yake itaondolewa kwa vitendo.

Wala sisemi kwamba vitendo hivyo ni kuandika barua kwa Waziri Mkuu kuomba msaada. Nasema juu ya vitendo vya viongozi wenyewe na wanachama wa TANU Ni juu ya viongozi kumfikia Maganga bin Musa kwa haraka kadri iwezekanavyo wasikitike pamoja naye kwa taabu aliyopata. Ila hiyo haitoshi. Ni juu yao kuita mkutano wa haraka wa Halmashauri yao, wazungumze juu ya shida ya Maganga bin Musa jinsi ya kumsaidia. Hivyo, pia haitoshi.

Ni juu yao kupita kwa wanachama na watu wengine katika kijiji chao na kuwashawishi kumsaidia Maganga bin Musa katika shida yake. Hivyo, pia haitoshi. Ni juu yao kuendelea hivyo hivyo mpaka shida ya Maganga Bin Musa imeondolewa kabisa kwa jitihada hiyo ya wanachama wa TANU na viongozi wao.

Nimetoa kuunguliwa nyumba kama mfano m moja tu wa shida zinazowafikia ndugu zetu kila siku. Lakini ziko shida za aina nyingi. Kuunguliwa, kufiwa, kuvuna, kupata chakula japo cha siku moja, shida kadha wa kadha za safarini, na shida za aina nyingi zinazowapata ndugu zetu kila siku. Ikiwa sisi ni viongozi wa watu, na Chama chetu ni cha watu, basi sisi hakuna shida yo yote ya watu ambayo twaweza kusema kuwa haituhusu.

TANU ndilo kundi moja katika nchi hii ambalo halina budi lijishughulishe na shida za kila mtu. Yapo makundi ya dini au madhehebu Fulani ya dini. Makundi hayo mara nyingi hushughulikana shida kama hizo nilizozitaja. Lakini kwa desturi hujishughulisha na shida za watu wa dini yao au madhehebu yao.

Kadhalika yako makundi ya makabila au ukoo, yanayoshughulika na shida za aina hiyo.

Lakini makundi hayo pia hushughulika na shida za makabila yao, au ukoo wao. TANU haina dini, au kabila au ukoo. TANU ni ya dini zote, na makabila yote na koo zote. Ni TANU peke yake, basi ambayo ina wajibu mkubwa kushughulika na shida za watu wa aina yo yote.

### SHIDA ZA JUMUIYA

Wakati mwingine huwa tukizungumza shida za Jumuiya, yaanisiyo shida za mtu mmoja mmoja. Ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba kwa kweli hizo ni shida za Jumuiya, siyo uzushi wetu wenyewe kwa faida yetu wenyewe. Mambo tunayo yazungumza katika mikutano yetu hayana budi yatokane na watu wenyewe huko vijijini kwao.

Tukishayazungumza na kuona jinsi ya kuondoa shida hizo hatuna budi turuditena kwa watu wenyewe kule vijijini tuzungumze upya shida hizo na jinsi tunavyofikiri shida hizo zaweza kuondolewa kama mawazo ya watu wenyewe yatakubaliana vema. La sivyo, tusikilize watu wenyewe wana mawazo gani.

Hatuna budi tuendelee na mazungumzo haya na watu wenyewe mpaka zipatikane nji za kuondoa shida zao ambazo ni zao na ni zetu pamoja. Baada ya hapo mipango itakuwa ni mipango ya raia wenyewe, siyo mipango waliyong'ang'anizwa na wakubwa kutoka juu kama ilivyokuwa kawaida ya Serikali ya Kikoloni.

Kwa njia hiyo watu wenyewe watajua jinsi ya kushughulika na wenda wazimu wachache ambao pengine watapenda kuchafua mipango ya kuondoa shida zao. Nimesema kuwa shida za Jumuiya hazina budi zitoke vijijini. Hii ni sheria nzuri lakini si amri ya Mungu.

**Itaendelea**



# Jamii

**Na Dk. Felician Kilahama**




# 'Ushoga na dhana ya kuoana jinsia moja. Je; ni halali? -1

NAMSHUKURU Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai pamoja na amani tuliyonayo nchini Tanzania. Licha ya changamoto nyingi za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kimazingira; lakini Mungu wetu aliye hai, yupo pamoja nasi siku zote. Hivyo tunapaswa kumshukuru na kumtukuza katika yote.

Kama sikosei, neno 'ushoga' siyo geni kwa Watanzania ambao, kwa namna moja au nyingine, wamewahi kulisikia au hata kulitamka. Miaka iliyopita (zamani), matumizi ya neon hilo, yalikuwa tofauti na ilivyo kwa majira 'ya sasa.'

Je; tunatumia vigezo gani tunayaainisha majira 'ya zamani' na jinsi yanavyotofautiana na majira ya 'ya sasa?

Kwa mtazamo na uelewa wangu na kwa kuzingatia hali halisi, naweza kusema kabla ya kupata Uhuru na baada ya kujitawala hadi miaka ya 1990: tunaweza kusema kipindi hicho ni 'majira ya zamani'.

Kuanzia miaka ya 1990 hadi sasa (2023), kukiita kipindi cha 'majira ya sasa.'

Iwe zamani au sasa, masuala ya sayansi/teknolojia; mila/desturi/utamaduni; siasa na mazingira hususan mabadiliko ya tabianchi, hayakwepeki kwa kumaanisha kwamba ni mambo yanayojitokeza katika vipindi vyote viwili tofauti ni kiwango cha mabadiliko.

Mathalani, sayansi/teknolojia hata zamani vilikuwepo ila kiwango cha mabadiliko kimeonekana kushika kasi sana katika miongo mitatu iliyopita: majira 'ya sasa'.

Kadhalika, kwenye masuala ya kijamii, utamaduni na mila/desturi zetu kuna mabadiliko makubwa sana.

Mfano, mila, desturi potofu na kandamizi hasa kwa wanawake na watoto, zimeendelea kutoweka. Bado masuala machache kama 'ukeketaji' na baadhi ya wazazi kutopenda watoto wao wapate elimu licha ya serikali kuamua watoto 'wasome bure' mpaka kidato cha sita, lakini hali bado ni 'kizungumkuti.' Katika siasa, pia kumekuwepo na mabadiliko hadi kuwepo kwa vyama vingi.

Zamani, msingi ulikuwa wa chama kimoja pamoja na filosofia/idiolojia za "Ujamaa na Kujitegemea" zilijengwa kwenye msingi wa 'binadamu wote ni sawa na Afrika ni moja' na kuzingatia 'utu' na 'heshima' kwa binadamu wote bila ya kuwepo kubaguana kwa aina yoyote ile. Hali ya mazingira ukilinganisha zamani na sasa, kasi ya kubadilika imekuwa kubwa sasa katika majira 'ya sasa,' mfano, 'mabadiliko ya tabianchi'.

Katika majira 'ya sasa,' masuala mengine yameibuka na kutishia heshima ya binadamu.

Mathalani, mihemko na kushabikia kwa kiasi kikubwa masuala yanayohusu "USHOGA".

Mambo kama haya yanasababisha kutokuelewana katika familia zetu, jamii na taifa kwa ujumla kwa sababu yanagusa sana 'imani', maadili na misingi ya uumbaji wa wanadamu: 'mume' na 'mke'.

Inafika mahali wengi tunajiuliza kulikoni katika majira 'ya sasa'? Kwa miongo miwili iliyopita suala hili limekuwa likipigiwa 'gitaa' kwa sauti kubwa ili wahusika 'kujinafasi wapendavyo.'

Katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu; Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (1981) inabainisha kuwa 'Shoga' ni jina linalotumiwa na wanawake Walio marafiki sana sana wakati wa kuitana au kujulishana kwa wengine. Mfano, fulani ni 'shoga' wangu kwa kumaanisha rafiki yake.

Vile vile, Kamusi inabainisha kuwa 'shoga' ni aina ya mwanamume anayefanya mambo ya kike; au 'hanithi/msenge/rambuza' kuashiria ni mwanaume asiye na uwezo wa kufanya tendo la ndoa. Kadhalika, Kamusi ya Kiingereza: inamtaja mwanaume anayefanya mambo ya kike kuwa ni 'gay': kumaanisha wanaume ambao wanavutiwa kufanya mapenzi ya jinsia moja. Kwa Kiingereza mwanamke anajulikana ni 'lesbian' hivyo, 'gay' na 'lesbian' ni wanaume/wanawake wanaohangaika na 'mapenzi' ya jinsia moja na kwa pamoja kujulikana kama 'homosexuals.'

Hii ni hali/dhana inayopingana na mahusiano ya watu wa jinsia tofauti yaani 'mume' na 'mke' (heterosexual) kama ilivyoainishwa tangu kuumbwa kwa binadamu wa kwanza, Adam na Hawa/Eva. Tangu zamani, urafiki kwa watu wa jinsia moja ulikuwepo, ninachofahamu ulikuwa wa Ki-Mungu kwamba watu tupendane, kama Mungu mwenyewe anavyotupenda. Hivyo, tulikuwa tunapendana na hata sasa inatakiwa iwe hiyo kutokana na agizo la kupendana kama ndugu wa tumbo moja (tukiwa sehemu ya uzao wa Adam na Hawa).

> **Mambo kama haya yanasababisha kutokuelewana katika familia zetu, jamii na taifa kwa ujumla kwa sababu yanagusa sana 'imani', maadili na misingi ya uumbaji wa wanadamu: 'mume' na 'mke'...**

Sasa dunia imechafuka yanayozuka sasa yanaashiria hali ilivyo ya 'machafuko' na yenye asili ya 'kishetani'.

Kinachoshangaza sana ni chimbuko la machafuko haya kutokana na 'mataifa' yenye hali tunayoiita ya maendeleo makubwa ya elimu, sayansi na teknolojia na utandawazi wa hali ya juu.

Mataifa kama Tanzania, yanakazana kujiletea maendeleo (kwa kurejea yaliyofanyika katika mataifa yaliyoendelea sana). Kimsingi, baadhi ya mataifa hayo yametawala Bara la Afrika: Katika harakati za kututawala, wakaanzisha shule (ili tuwe na elimu/kuongeza maarifa).

Kadhalika, wakaanza kujenga baadhi ya miundombinu kama Reli ya Kati (Dar es Salaam mpaka Mwanza na Kigoma pia mpaka Mpanda mkoni Katavi. Vile vile, wakajenga bandari, barabara na huduma za afya, mfano, hospitali na vituo vya afya/zahanati na mengineyo. Juhudi hizo zililenga kuandaa jamii ya Watanzania (wakati ule Watanganyika na Wazanzibari) kumudu maisha kwa kuwa na afya njema, akili/maarifa na kufanya maamuzi sahihi.

Haikupita muda mrefu, Wamissionari kutoka mataifa yaliyoendelea wakafika nchini mwetu zaidi ya miaka 100 iliyopita kwa kusudi za kueneza Injili (habari njema kwa watu wote). Kutokana na hatua hiyo, Watanzania tukamjua Mungu wa kweli aliye hai, hivyo kuachana na maagano/ibada za kijadi/kimila.

Katika kumjua Mungu wa kweli, ndipo pia tulipofahamu kuwa yeye ndiye aliyeumba dunia na vyote viijazavyo wakiwemo binadamu. Maandiko Matakatifu yanathibitisha kuwa Mungu alimuumba binadamu kwa mfano na sura yake: "Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai." (Mwanzo 2:6).

Baada ya kumuumba Adam, Mungu akaona amekuwa mpweke: akasema 'si vema huyo 'mtu' awe peke-yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye'. Ndipo Bwana Mungu akamletea Adam usingizi mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja akafunika nyama mahali pake, na ule ubavu alioutwaa katika Adamu, Bwana Mungu akaufanya mwanamke akamleta kwa Adam.

Hivyo, Mungu akaumba jinsia mbili ya 'kiume' na 'kike' na Adam akawa 'mzaliwa wa kwanza' wakati huo msaidizi wake akawa 'mzaliwa wa pili'. Bwana Mungu akawabariki akawaambia 'zaeni muongezeke na kuijaza nchi.' Mzaliwa wa kwanza 'Adam' akapewa amri ya kumiliki na kutawala na kuisimamia familia yake ipasavyo wakati huo mzaliwa wa pili 'Hawa' akiwa msaidizi wake halisi.

Kwa msingi huo, Mwenyezi Mungu ndiye asili na msingi wa familia zetu; mwanaume aishi na mwanamke na wazae na kuongezeka (zawadi ya watoto kutoka kwa muumbaji wetu).

Kwa kuwa 'Hawa' alitwaliwa katika mwanaume, hivyo mwanaume atawaacha wazazi wake (baba na mama); naye ataambatana na 'mkewe' (mwanamke), na hao wawili watakuwa 'mwili mmoja.'

Sasa taswira za 'mwanaume kumuoa 'mwanaume' (gays) au 'mwanamke'kumuoa 'mwanamke' (lesbian), zinatoka wapi?

**Itaendelea sehemu ya pili.**

Elimu



# Ruangwa yavuka lengo ujenzi sh

**Na Mwandishi Wetu**

SERA ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ni kujenga shule ya sekondari katika kila kata nchi nzima. Hata hivyo, wakati utekelezaji wa sera hii ukiendelea, tayari Wilaya Ruangwa mkoani Lindi, imevuka lengo hilo kama Mwandishi Wetu, Abdul Mitumba, anavyoandika katika makala hii.

WILAYA ya Ruangwa mkoani Lindi, mpaka kufikia mwaka huu, tayari imejenga shule za sekondari 24 katika kata zake 22, ikiwa tayari imekwisha vuka shule mbili ya lengo la kisera la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia la kujenga shule ya sekondari katika kila kata.

**Nini siri ya mafanikio?**

Mpaka ilipofika mwaka 2010, Wilaya ya Ruangwa iliyokuwa na kata 15 kw wakati huo, ilikuwa na shule moja tu ya Sekondari ya Mbekenyera.

Kwa sasa shule hiyo inapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi sita pamoja na sekondari za Nkowe High School ya Mchepuo wa Sayansi ya Kilimo, Ruangwa High School (Mchepuo wa Biashara) na Hawa Mchopa (Mchepuo wa Sanaa).

Nyingjne ni Lucas Maria Girls High School na Ruangwa Girls High School ambazo sasa zinakamilisha idadi ya shule 27 za sekondari wilayani Ruangwa.

Tangu wakati huo, wilaya hiyo imekuwa ikijenga shule moja baada ya nyingine hadi kufikia 27 mwaka huu, ambapo kati ya hizo, zipo sekondari mbili zinazotarajiwa kufunguliwa wakati wowote kuanzia sasa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Andrew Chikongwe, anasema baada ya Mbekenyera Sekondari, wakazi wa Wilaya ya Ruangwa walijifunga kibwewe na kuanza kujenga shule kwa utaratibu wa wananchi kujitolea katika hatua za awali na serikali kumalizia majengo.

Anasema utaratibu huo umesaidia kupatikana kwa shule hizo kiasi cha kuvukalengo la Sera ya Elimu, ambapo Kata ya Narungombe ina sekondari mbili, Kata ya Nachingwea inazo mbili na Kata ya Mnacho, pia ina sekondari mbili.

Afisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Ruangwa, Mwalimu Haule, anasema baada ya Mbekenyera Sekondari, zikafuata Nkowe Sekondari na sasa zimejengwa Sekondari za Kata za Mbwemkuru na Nanganga wakati ile ya Wasichana ya Mkoa wa Lindi yenye hadhi ya kitaifa, pia ikijengwa Ruangwa Mjini na itakapokamilika, itagharimu zaidi ya Sh.bilioni 1.1.

Mwalimu Haule anasema, ujenzi wa Sekondari za Nanganga na Mbwemkuru, unasimamiwa na Halmashauri yake baada ya kupokea fedha Sh. milioni 940 za awali kutoka Ofisi ya Rais Tawala za

**Baada ya kukamilika kwa ujenzi, kiasi kingine cha Sh. milioni 130 kilitolewa kujenga na kukamilisha nyumba za walimu na kununua vifaa kwa ajili ya chumba cha kompyuta...**



# ule za sekondari kila kata



Mikoa na Srikali za Mitaa (Tamisemi) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari nchini (SEQUIP).

Afisa Mtendaji wa Kata ya Nanganga (ambaye kwa sasa amehamishiwa Kata ya Mandawa), Saidi Ng'itu, anasema ujenzi wa shule hiyo mpya, ulihusisha madarasa manane, jengo moja la utawala, chumba cha kompyuta (ICT), maktaba moja na vyoo matundu 20.

Amesema majengo karibu yote yamekamilika ujenzi wake na kwamba anajivunia kuona wananchi wa Kata ya Nanganga, wameshiriki kikamilifu katika shughuli zote muhimu, ikiwemo kujaza kifusi katika vyumba vyote, kusomba mchanga na kuchota maji na kuyafikisha eneo la ujenzi na hatimaye kukamilika kwa ujenzi.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Nanganga, Shabani Kambona, anasema mradi mzima umegharimu Sh. milioni 600 hadi utakapokamilika na kwamba Sh. milioni 470, zilitolewa awali.

"Baada ya kukamilika kwa ujenzi, kiasi kingine cha Sh. milioni 130 kilitolewa kujenga na kukamilisha nyumba za walimu na kununua vifaa kwa ajili ya chumba cha kompyuta," anasema Kambona.

Ameongeza kuwa, sambamba na hayo, mradi pia umehusisha ujenzi wa tangi la maji lenye uwezo wa kuhifadhi lita 10,000, nguzo ya kuweka tangi, ujenzi wa miundombinu ya kunawa mikono na miundombinu ya kuvuna na kuunganisha nishati yenyewe.

Hata hivyo, gazeti la Mwelekeo, linatambua kuwa ujenzi wa shule hizo, unahusisha nchi nzima ambapo serikali ilipanga kutekeleza mradi wa kujenga shule za sekondari 214 kupitia mradi wa SEQUIP ambapo Tamisemi katika awamu ya kwanza, ilisambaza Sh. bilioni 100.58 kwa ajili ya ujenzi wa shule hizo ambazo zimejengwa kwenye kata za majimbo yote yaliyokuwa hayana shule nchini.

Kadhalika, mradi huo umepeleka Sh. bilioni 30 nyingine kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari mpya za wasichana kwenye mikoa 10 ambapo kila mkoa umepata shule moja ya wasichana kwa ajili ya mchepuo wa sayansi ya kidato cha kwanza hadi sita.

Mradi huu umelenga maeneo ya kipaumbele ambapo zimejengwa shule katika kata zisizo na shule au idadi kubwa ya wanafunzi katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, ambapo gharama halisi ya kila shule moja ni Sh. bilioni 4.0 hadi kukamilika kwake.

Taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Ofisi ya Rais- Tamisemi, Nteghenjwa Hosseah, imefafanua kuwa, fedha zilizotolewa zinapaswa kutumika katika kipindi kilichopangwa na kwamba mradi unaojulikana kama `Secondary Education Quality Improvement Program (SEQUIP).

Hosseah anasema SEQUIP ni mradi wa kimkakati unaogharimiwa na serikali kwa mkopo wa takribani Sh. trilion 1.1 kutoka Benki ya Dunia (WB).

Siasa



# Rais ameonyesha ukomavu, kazi kwenu wapinzani jengeni hoja - 2

**Na Dk. Felician Kilahama**

HUU ni mwendelezo wa sehemu ya kwanza wa makala iliyohusu hali ya kisiasa hapa nchini kwa kuzingatia mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Katika sehemu ya kwanza, niliweka bayana kuhusu kinachojiri hasa 'ruksa' kwa vyama vya siasa kuendesha mikutano ya kisiasa bila vipingamizi.

Sehemu hii ya pili, inatoa ufafanuzi wa masuala ya msingi ambayo tukifanikiwa, tutakuwa tumejenga 'demokrasia' ya kweli kwa manufaa ya wote.

Januari 25, mwaka huu, baadhi ya vyombo vya habari vilimkariri Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, akiwataka viongozi wa Chama na Serikali kuwajibika na kwamba viongozi 'legelege' sasa hawana nafasi.

Mtendaji huyo wa CCM, pia alimtaka kila kiongozi kujitathmini ipasavyo kwa kuzingatia kuwa fursa za kuchekeana zinaelekea kuwa finyu. Kwa mujibu wa vyombo vya habari, Chongolo alitoa maagizo hayo alipokuwa akizungumza na viongozi na baadhi ya wanachama wa chama hicho mjini Dodoma, alipokuwa akizungumza katika mapokezi ya 'Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa' ya CCM.

Siku iliyofuata, kupitia vituo vya runinga na radio, Chongolo alisikika akitoa kauli inayofanana na mtazamo wangu kwamba Watanzania walio wengi, sasa wanahitaji miundombinu bora kwa maana ya barabara safi na zinazopitika mwaka mzima vijijini na mijini.

Hali kadhalika, huduma za maji, elimu na afya zikiwa za uhakika na endelevu.

Lakini pia wanahitaji vitendea kazi vya kisasa katika shule na zahanati,vituo vya afya na hospitali zote, zikiwemo za serikali na watu binafsi.

Kwa kuwa tunaishi katika ulimwengu wa kidijitali, upatikanaji wa mawasiliano ya uhakika mijini na huko vijijini sasa si tena suala la kusubiri. Lakini wakati huduma hizo zinahitajika sana, pia lazima kuwe na mikakati ya kuhakikisha kuwa zinapatikana kwa gharama nafuu kwa watumiaji badala ya kuwa mkomoeni.

Uzoefu unaonyesha kuwa wanaomiliki mitandao ya simu wanapata faida kubwa sana kila mwaka (mabilioni ya pesa). wakati mitandao hiyo ikitumia gharama kubwa kwa matangazo ya mara kwa mara kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Kadhalika, huweka matangazo husika sehemu mbalimbali za mijini na vijijini.

Wanatangaza huduma zao kupitia huduma za matangazo ya nje yakiwemo mabango (posters) na "billboards" na hata magari yenye-vipaza sauti wanayopita nayo mitaani wakitangaza huduma hizo.

Haya yote yanamuongezea gharama kubwa mtumiaji wa huduma za mawasiliano na teknolojia husika.

Hata kama vyombo vya habari na waigizaji watanufaika kutokana na matangazo; lakini ukweli ni kwamba watumiaji wa huduma hizo ndiyo wanaobeba mzigo wa gharama kubwa.

Hivi kwa nini mawasiliano yawe 'mwiba' kwa mtumiaji wa huduma, kunakosababishwa na gharama za 'vifurushi' vya kuongea au/na matumizi ya 'intanenti' kwisha haraka huku malipo yake yakiwa juu; au ndiyo mifumo ya kibepari.

Pamoja na hayo, huduma za kilimo na ufugaji zinapaswa kuboreshwa zaidi mkazo ukiwa katika kuwapata watumishi/wataalam wa kutosha na wanaowajibika ipasavyo.

Jitihada lazima zifanyike ili watumishi wa sekta zote hasa za elimu, afya, maji, kilimo na mifugo,kuhakikisha kuwa wanapewa vifaa muhimu vya kufanyia kazi zao.

Maliasili na utalii, na maendeleo/ustawi wa jamii. Nchi yetu itaendelezwa na wenye moyo, wazalendo na wenye uchungu wa rasilimali tulizo nazo. Ardhi itumiwe vizuri na kuzalisha mazao kitaalam na kwa tija kubwa.

Lakini pia wafugaji wakisimamiwa na kuongozwa ipasavyo, hawatazurura ovyo kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine kwa lengo la kutafuta malisho na maji kwa mifugo. Kwa hiyo, wanapaswa kumilikishwa maeneo ya kufugia mifugo na wawajibike kuyasimamia na kuyatunza ipasavyo na kuzalisha bidhaa zitokanazo na mifugo kwa weledi mkubwa bila kuharibu mazingira.

Katibu Mkuu wa CCM aliposema 'Watanzania wanataka barabara zilizoimarika hadi vijijini; wapate huduma za maji, elimu na afya bila kuhangaishwa' alimaanisha kweli.

Haya yote yanahitaji watumishi waliodhamiria kuwaletea maendeleo endelevu Watanzania. Watanzania tunataka 'miundombinu' imara, mawasiliano yawe rahisi na kwa gharama rafiki.

Wakulima kwa upande wao, wapate pembejeo za kilimo na mifugo kwa wakati na gharama nafuu.

Kuwe na watumishi wa serikali wanaotimiza wajibu wao ipasavyo bila kusukumwasukumwa. Kujitawala ni kufanya kazi kwa bidii na kutimiza wajibu kwa haki na amani. Watumishi wa serikali wachukie rushwa na 'roho' za kupenda hongo/zawadi na badala yake, watende haki wakati wote.

Hali kadhalika wawahudumia Watanzania wote bila ubaguzi wa aina yoyote ile na 'fitina' iwe mwiko.

Kuyatimiza haya yote hakuhitaji 'katiba mpya' wala 'demokrasia' kama ilivyo katika nchi zenye maendeleo makubwa kiuchumi na kijamii.

Tunachohitaji zaidi ni dhamira njema kutoka kwa viongozi wanaofanya maamuzi na watunga sera.

Katiba na demokrasia vinaweza kuwepo lakini bado 'kukawa na kizungumkuti.'

Shughuli za umma zilifanyika kwa nia njema na kwa kufuatana na sheria na kanuni zilizokuwa zikiboreshwa mara kwa mara ili kutenda haki.

Kinachosumbua nyakati hizi ni 'roho' za ubinafsi na kujipenda zaidi kuliko 'kumpenda jirani kama unavyojipenda.'

Maslahi binafsi na migongano ya kimaslahi kwa watumishi wa umma, ni changamoto kubwa sana.

Kama 'Katiba mpya' na 'demokrasia' vitasaidia kuondoa 'roho' hizo miongoni mwa watumishi wa umma na wakawajibika ipasavyo bila kujali maslahi binafsi, basi tukazane hali iwe hivyo. Kinyume chake, itatuchukua muda mrefu sana kuyashuhudia mambo muhimu ambayo Watanzania walio wengi, wana kiu ya kuyaona yamefanyika kama Katibu Mkuu wa CCM alivyoainisha.

Kwa maneno mengine, tumethubutu na tumeishaona inawezekana, sasa ni kuongeza kasi katika kuwaletea maendeleo Watanzania wote mijini na hasa vijijini.

Tumuombe Mwenyezi Mungu aliye muweza wa yote 'Alpha na Omega'; atuondolee 'mageule' ndani ya mioyo yetu na hasa kwa viongozi wa ngazi zote ili waweze kuwatumikia wananchi kwa uaminifu mkubwa wakitenda haki kwa faida ya wote. Sasa Tanzania 'kumekucha' tunahitaji maendeleo ya kweli na yenye tija kwa wote. Baada ya 'mzinga' kufunuliwa, nyuki ni wengi kila mahali wanatafuta malighafi ya kutengeneza asali ikiwemo 'chavua'(pollen) na 'mbochi'(nectar). Je, nini kitatokea iwapo 'ukame' utazidi kuongezeka?

Naamini hali ya hewa itakuwa nzuri ili vyama vyote vya siasa viweze kutupa 'karata' zao vikiweka bayana hoja zenye 'manufaa' kwa amani na utulivu mkubwa.

> **Kuyatimiza haya yote hakuhitaji 'katiba mpya' wala 'demokrasia' kama ilivyo katika nchi zenye maendeleo makubwa kiuchumi na kijamii...**

# Uchumi





# Kamati Mkoa wa Songwe yakagua barabara kujiridhisha ubora, matumizi sahihi ya fedha

**Na Lauden Mwambona, Songwe**

KAMATI ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Songwe, imekagua baadhi ya miradi ya barabara inayosimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads).

Kamati hiyo ilifanya ziara hiyo Februari 23 hadi Februari 26, mwaka huu, lengo likiwa ni kufuatilia fedha nyingi zinazoletwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya miradi ya maendeleo iwapo zinatumika kama iliyokusudiwa na kwa thamani yake halisi.

Kwa kawaida, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa, ni Mkuu wa Mkoa, lakini ujumbe uliofanya kazi hiyo, uliongozwa na Katibu Tawala Mkoa huo, Happiness Seneda ambaye alikuwa Kaimu Mwenyekiti kutokana na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wakati huo, Waziri Kindamba, kuwa safarini.

Kindamba kwa sasa ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga huku nafasi yake ikichukuliwa na Dk. Francis Michael.

Kamati hiyo ilianza kazi katika Wilaya ya Mbozi kwa kukagua ujenzi wa daraja kwenye barabara inayounganisha Wilaya za Mbozi na Ileje kupitia Hasamba Izilya hadi Itumba Ileje.

Ujenzi huo umegharibu zaidi ya Sh. milioni 136.4 na pia walikagua barabara ya Shigamba Itumba hadi Isongole ambayo inakarabatiwa

> **Kindamba kwa sasa ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga huku nafasi yake ikichukuliwa na Dk. Francis Michael....**

kwa gharama ya Sh. milioni 686.02 na hatimaye Kamati ilikwenda kwenye barabara ya Itumba Shigamba hadi Ibaba inayokarabatiwa kwa Sh. milioni 418.7.

Ikiwa wilayani Ileje, Kamati ilikagua pia matengenezo ya kawaida barabara ya kutoka Ibungu hadi Kafwafwa ambayo inatarajiwa kutumia zaidi ya Sh. bilioni 1.216.

Siku ILIYOFUATA, kamati hiyo ilielekea wilayani Songwe ambako walikagua miradi mitatu tofauti inayoendelea kutengenezwa na wakandarasi watatu tofauti katika barabara ya Chang'ombe kwenda Patamela na mradi mmoja katika barabara ya kutoka Saza kwenda Kapalala.

Miradi yote minne ina thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.92.

Ukaguzi huo wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Songwe, ulimazika kwa siku ya tatu ambayo ilifanya kazi katika Wilaya ya Momba kwa kutembelea barabara ya kuanzia Mlowo hadi hadi Kamsamba ambayo inakarabatiwa kwa gharama ya Sh. milioni 765.15 na ile ya kuanzia Igamba Msangano-Chitete hadi Utambalila inayofanyiwa matengenezo kwa gharama ya Sh. milioni 530.

Akizungumza siri ya ukaguzi huo, Katibu Tawala Mkoa wa Songwe anasema ni kufuatilia fedha nyingi zinazoletwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Samia Suluhu Hassan kwa miradi ya maendeleo.

Anatoa mfano kwa fedha zilizoletwa kwa Tanroads pekee katika kipindi cha Rais Samia kwamba ni zaidi ya Sh. bilioni 27.5 na kwamba ni jukumu lao kufuatilia kujua kama fedha hizo zote zinafanya kazi iliyokusudiwa na kuangalia ubora na kama kazi zitamalizika kwa wakati.

Akitoa taarifa , Kaimu Meneja wa Tanroads Mkoa, Injinia Suleiman Bishanga, anasema miradi iliyokaguliwa ni sehemu ya miradi mingi inayoendelea kufanyika katika barabara mbalimbali mkoani humo.

Anasema pamoja na kuwapo mvua nyingi, Serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia imezikarabati barabara hizo na zinapitika wakati wote.

Kauli hiyo inaungwa mkono na Mkuu wa Wilaya Momba, Fakii Lulandala ambaye anaiambia kamati hiyo kwamba barabara zote zinapitika vizuri.

Naye mkazi wa Kijiji cha Msangano, Eliagali Simkazi, ambako unafanyika ukarabati wa kuweka tuta barabara eneo la Msangano, anaishukuru serikali kwa kazi kubwa inayofanyika kuhusu barabara.

Anasema kwa kipindi kirefu, barabara hiyo ilikuwa ikikatika kipindi cha mvua, lakini sasa serikali ipo kazini.

Naye mkandarasi anayejenga eneo hilo, Udan Miradi, anasema wanaifanya kazi kwa ubora na wataikabidhi kabla ya kumaliza siku za mkataba Juni 30, mwaka huu. Kwa ujumla, Mkoa wa Songwe ni kitinda mimba, yaani ni mkoa wa mwisho kuundwa hapa nchini na hivyo una changamoto nyingi zikiwamo za barabara ambazo kwa mwaka huu, zinatajwa kwamba zimeboreshwa kuliko miaka iliyopita. Wakazi wa Mkoa wa Songwe wanajishughulisha na mambo mengi ya kiuchumi yakiwamo ya madini, uvuvi, mifugo na kilimo na hivyo wanahitaji barabara bora za lami, lakini kwa kuanzia barabara za changarawe zinapitika.

Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Solomon Itunda anamshukuru Rais Dk. Samia kwa fedha nyingi za barabara.

Itunda pia anapongeza hatua ya kufanya upembuzi yakinifu barabara ya kutoka Mbalizi mkoani Mbeya hadi Mkwajuni mkoani Songwe ikiwa ni maandalizi ya kujenga kiwango cha lami.

Kaimu Meneja wa Tanroads, anasema serikali ipo kuboresha barabara zikiwamo za kiwango cha lami.

Anataja baadhi ya barabara ambazo tayari zabuni zilishatangazwa kuwa ni pamoja na ile barabara za kutoka Isongole hadi Isoko wilayani Ileje na barabara kuu ya Tanzania- Zambia maarufu kwa jina la Tanzam kutoka Igawa hadi Tunduma.





## Biashara



# Wajue aina tano ya wateja na sifa zao

**Na Mwandishi Wetu**

MTEJA kwa tafsiri rahisi, ni mnunuzi wa bidhaa kutoka kwa mfanyabiashara.

Hivyo, kuna uhusiano mkubwa kati ya mfanyabiashara na mteja.

Aidha, mteja ni chanzo kikubwa cha mapato katika biashara yoyote.

Unaweza kuwa na bidhaa au huduma bora, mfano; mhasibu mahiri au msimamizi bora, lakini hutaambulia chochote kama hutakuwa na mfereji wa mapato katika biashara yako.

Mfereji huu wa mapato katika biashara yoyote, hutokana moja kwa moja na mauzo. Ndiyo maana wataalamu wanakubaliana kuwa bila mauzo, hakuna mapato na bila mapato, biashara itaanguka. Hakuna kitakachofanyika cha maendeleo kwenye biashara bila mauzo. Aina tano za wateja katika biashara

**1. Mteja mshirika**

Huyu ni mtumiaji wa bidhaa na huduma za mfanyabiashara ingawa hana uamuzi wa mwisho kwenye ununuzi. Mteja wa aina hii, hahusiki na usimamizi wa fedha ila ni kiungo muhimu kwa mfanyabiashara katika kufanikisha mauzo ya bidhaa au huduma.

Licha ya kwamba uamuzi wa mwisho wa kununua kutoka kwa mfanyabiashara hahusiki, lakini anaweza kuwa na mchango kwenye matokeo ya mauzo.

Hivyo, hakikisha mteja wa aina hii, unajenga naye uaminifu na kukubalika.

Chunga kupoteza muda kwa mteja mshirika, mtumie zaidi kama chanzo na hazina ya kupata taarifa muhimu za kampuni unayotaka kufanya nayo biashara.

Hazina hii itakupa nafasi ya kujitofautisha na washindani wako kwenye kampuni hiyo. Kinachouza, ni tofauti na siyo kufanana.

Kumbuka kuuliza maswali stahiki mwanzoni kujua nani ndiye mwenye maamuzi ya mwisho na ni nani ndiye mteja mshirika. Hii itapunguzia urasimu na kuokoa muda.

Hata hivyo, kumbuka pia hata kama hawana maamuzi ya mwisho, wana nguvu ya turufu na iwapo watakukataa, itakuwa ni changamoto kwa uamuzi wa mwisho kufanywa na bosi.

Aidha, kukukataa kwa mteja mshirika kila wakati, haimaanishi akisema ndiyo biashara itakamilika. Chunga kupoteza muda kwa mteja mshirika kwa kuwa ndiyo yake haikamilishi biashara. Zaidi watumie kama chanzo na hazina ya kupata taarifa muhimu za kampuni unayotaka kufanya nayo biashara.

**2. Mteja wa Nje:**

Huyu ni mteja au kampuni anayehitaji bidhaa na huduma zako. Ndiye mnunuzi mkubwa wa thamani yako na chanzo cha hazina ya mfereji wako wa mapato. Kila mwaka anatenga bajeti kwa ajili ya bidhaa na huduma kama zako. Ukitoa suluhisho kwa matarajio na mahitaji yake, hasiti kukupa gawio kutoka kwenye bajet hiyo.

Mteja wa nje hawajibiki kwako kukupa gawio hili. Utahitaji kuwasilisha bidhaa au huduma bora zaidi ya washindani wako. Ukimjengea uaminifu na akathamini kile unachouza, ni rahisi kuwazidi washindani wako.

**3. Mteja wa Ndani**

Hawa ni wafanyakazi wenzako na mameneja ndani ya kampuni uliyoajiriwa. Wanakujenga na kukufanya uonekane mzuri na wateja wa nje. Tambua mchango wao na uwaheshimu kadiri uwezavyo.

Kwa bahati mbaya, ni waathirika wakuu wa malalamiko yako kila linapoharibika jambo. Utasikia idara ya uchukuzi wameniangusha, mhasibu kachelewasha risiti au maudhi na mengineyo.

Uhusiano baina ya wafanyakazi ndani ya kampuni ukidorora, unatoa twasira mbaya kwa wateja wa nje. Wajibika kila wakati kwa kuwa ni balozi mzuri wa kampuni uliyoajiriwa. Kubali kuwajibika kwa kila jambo. Usimrushie mwingine lawama. Tishio kwa kampuni siyo ushindani kutoka nje, bali ni mgogoro wa ndani kwa ndani.

> **Kwa bahati mbaya, ni waathirika wakuu wa malalamiko yako kila linapoharibika jambo...**

Tambua kundi lingine la wateja wa ndani ni familia yako, mke au mume, wazazi na wanao. Na wao pia wanaostahili kupewa heshima wakati wote.

**4. Mteja wa kila siku**

Hawa ni lulu na johari katika biashara yako. Kuna uwezekano mkubwa wa kupata kazi zaidi ya mara moja na hata kazi nyingine tofauti na ya awali ikiwa utatoa huduma bora. Wakishatambua ubora wako, hawana haja tena ya kukuchunguza na kukuhoji, bali kazi zitakuwa zinatiririka kwako. Na kadiri kazi inavyoongezeka ama ya kuuza bidhaa au kutoa huduma, ndivyo mfereji wa mapato unavyongezeka.

Kuwa na mteja wa kuendelea kunapunguza sana gharama ya uendeshaji. Wataalamu wa mauzo wanasema kubaki na mteja, haina gharama kama kumpata mteja mwingine mbadala wa yule aliyekukimbia. Baadhi wanasema gharama yake ni zaidi ya mara tano.

Hivyo basi, hakikisha mteja uliyenaye, haondoki. Uhakika ni kumwacha na furaha kila unapofanya naye biashara. Kila unapopata fursa ya kufanya kazi, timiza zaidi ya kile ulichoahidi kwenye makubaliano. Hii ndiyo siri ya mtenda kwenye kumbakisha mteja wako.

**5. Mteja Mtoro**

Hawa ni wateja wa zamani ambao wamekukimbia. Aidha, umewasahau au waliudhika na jambo wakati wa nyuma. Wajue, kisha wafuate ujue changamoto iliyopo na utatue. Weka kiburi kando, wewe ndiye mhitaji zaidi yao. Tafuta ruhusa ya kurekebisha changamoto hiyo. Na ukipata, jitahidi kurekebisha hali hiyo. Bila shaka ukimridhisha mteja huyu, atarudi kwa kishindo na kukujaza fedha kwenye mfereji wa mapato.

Amini usiamani, wakirudi huwa ni watiifu au zaidi ya mwanzo.

Biashara nyingi hushuka kutokana na kusahauliwa tabaka hili la wateja. Na kadiri unavyowapoteza, ndivyo wanavyozidi kusambaza sumu kwa wengine. Usipochunga, madhara yake yatakuwa makubwa zaidi.

HABARI KUTOKA ZANZIBAR

# Kijana kortini kwa kuingia nyumba ya watu bila ridhaa

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Kijichi Wilaya ya Magharibi A Unguja, Said Khamis Haji (20), amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya Mkoa wa Mwanakwerekwe kujibu shitaka la kuingia katika nyumba ya watu bila ya ridhaa ya mmiliki wa nyumba hiyo.

Ilidaiwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashitaka Koplo Rajab Mussa mbele ya Hakimu Saumu Kihio, kuwa mshtakiwa huyo bila halali, aliingia ndani ya nyumba anayoishi Subira Abdalla Hassan, kwa nia ya kutenda kosa la wizi, jambo ambalo ni kosa kisheria.

Koplo Rajab alidai kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Januari 17, mwaka huu saa 1:30 asubuhi eneo la Kijichi ambalo ni kinyume cha kifungu 296 (1) (a) (b) (2) cha Sheria Namba 6 ya mwaka 2018 Sheria za Zanzibar.

Hata hivyo, mshtakiwa alikana shitaka hilo na kuiomba Mahakama impatie dhamana.

Mahakama ilimtaka mshtakiwa kujidhamini mwenyewe kwa Sh. 100,000 za maandishi na wadhamini wawili kwa kila mmoja kulipa kiasi hicho cha fedha pamoja na vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na barua ya Sheha.




MKUU wa Operesheni ya Kampuni ya Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa, Philemon Azer, akizungumza na wafanyakazi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar katika mafunzo ya kuwajengea uwezo juu ya uendeshaji wa kutoa huduma katika Uwanja wa Ndege wa Terminal III. Picha: (Mpigapicha Wetu)

# ACT-Wazalendo yakunwa juhudi za wanawake Z`bar

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo Tanzania Bara, Dorothy Msemo, amefurahishwa na juhudi za wanawake wa Zanzibar wanavyoendelea kuwa imara kuitetea demokrasia ya kweli hapa visiwani humu.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja mwishoni mwa wiki iliyopita, Dorothy alisema wanawake ni sehemu kubwa katika kuleta demokrasia ya kweli na kuwataka waendelee kuisimamia.

> **Ninyi ni mfano bora na wa kuigwa katika kulisimamia hilo...**

Alisema kutokana na juhudi wanazochukua, wamekuwa mfano bora kuhakikisha mapambano yao kuhusu demokrasia inalindwa.

"Ninyi ni mfano bora na wa kuigwa katika kulisimamia hilo, na sisi wanawake wa Tanzania Bara tumekuwa tukijifunza kutoka kwenu", alisema Msemo.

Aidha, aliwataka waendelee kuwa na moyo huo huo wa kuhakikisha nchi yao inapata demokrasia ya kweli kwa maendeleo yao na vizazi vijavyo.

Alifafanua kuwa nchi bila kuwa na demokrasia ya kweli, hushindwa hata kupata maendeleo na kuingia katika mifarakano isiyo na tija kwa kizazi chao.

Hivyo alisema akiwa ni Makamu Mwenyekiti mwanamke, amevutiwa kwa kiasi kikubwa uwepo wa wanawake wengi katika mkutano huo ambao unaonesha wazi jinsi wanavyokiunga mkono chama hicho.

# Ukongoroni na Charawe watakiwa kuwa na subira

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Suleiman Hassan Makame, amewataka wananchi wa Vijiji vya Ukongoroni na Charawe visiwani humu, kuwa na subira juu ya utekelezaji wa ahadi zilitolewa na viongozi wao

Aidha, Makame amewataka wananchi wa vijiji hivyo kuondoa mawazo kwamba vijiji vyao vimetengwa.


Akizungumza na wananchi hao katika kikao cha pamoja cha kuzungumzia kero mbalimbali zinazowakabili wananchi hao, Makame alisema kuchelewa kutekelezewa kwa ahadi wanazoahidiwa, siyo kwamba wametengwa, bali ni jambo tu la muda.

Alifafanua kwamba kila mmoja anapaswa kujua kwamba visiwa vya Zanzibar baada ya kutoka kwenye mikono ya ukoloni waliwacha katika madhila makubwa yaliyosababisha kujenga mazingira magumu katika maeneo mbalimbali ya visiwa vya Unguja na Pemba. Hivyo alisema ahadi za viongozi bado zitabaki zile zile na alizotoa Rais aliyemaliza muda wake, Dk. Ali Mohamed Shein.

"Kwa hiyo, toeni katika vichwa vyenu kwamba wana-Ukongoroni na Charawe, mmetengwa kwani ahadi zitatekelezwa", alisema. Waziri Makame aliyasema hayo baada ya baadhi ya wananchi wa vijiji hivyo kudai kwamba vijiji vyao vimetebngwa kutokana na kuahidiwa ahadi nyingi ambazo hazijatekelezwa.

Wakizungumza mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid, baadhi ya wananchi hao, Mohammed Hassan Ame, wa Ukongoroni na Tendani Mlenge Miraji walisema kwa muda sasa vijiji vyao vimekuwa vikiahidiwa, lakini ahadi hazitekelezwi, jambo ambalo linawafanya wajione kama wametengwa.

Walisema katika vijiji hivyo, wana kero ya barabara ambayo licha ya kupitia Marais tofauti, lakini bado haijatekelezwa, jambo ambalo walitaka kupitia kikao hicho wapatiwe ufumbuzi wa lini barabara hiyo itajengwa. Akizungumzia suala hilo, Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Mohammed Salum, alisema barabara hiyo ni moja ya barararabara mbili ambazo Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekuwa akizizungumzia kila ambapo wanakutana ikiwemo na ile ya Uzi Ng'ambwa. Alisema amekuwa akizungumzia kutokana na kwamba barabara hizo zimekuwa na ahadi ya muda mrefu. "Sasa mimi nakwambieni, muaminini sana Rais Mwinyi hadi yake ipo pale pale na ndani ya kipindi hiki mpaka tukifika mwaka 2025 Mheshimiwa Rais amesema barabara zote tulizoziahidi zote ziwe zimeshajengwa, ambazo zinakaribia kilomita 725 ambazo haijawahi kutokea hata mwaka mmoja toka Zanzibar iundwe", alisema. Alisema huko nyuma baada ya miaka mitano, walikuwa wanaweza kujenga kilomita 60 , lakini ndani ya kipindi hiki barabara zote zitajengwa tena kwa kiwango cha lami.


HE! MBONA RAFIKI YETU ANAIMIMINA MIUNO YA NGUVU VILE MTAANI
MTOTO WAKE AMEPATA BAHATI YA KUPATA NAFASI KATI WALE WATOTO 22,000 WALIOPEWA OFA NA RAIS WETU DK SAMIA SULUHU HASANI YA KUSOMA KATIKA VYUO VYA UFUNDI BURE KWA KUWA WALIFELI DARASA LA SABA NA KIDATO CHA NNE
ASANTE MAMAAA... UBARIKIWE
Katuniz
KIMWELEKEO
@Muhidini Msamba
+255656122770
HOFA HII SIWEZI NIKAIACHIA IPITE LAZIMA NIKAFATE UTARATIBU ILI MWANANGU AKASOMEE UFUNDI MAANA SHULENI ALIPATA BUYU LA NGUVU
UNASEMA KWELI MZEE KITAMBI MIYEYUSHO AU UNANIDANGANYA KUWA WATOTO WETU WALIO FELI WATASOMA BURE KWENYE VYUO VYA UFUNDI
SASA ENDELEA KUZUBAA ZUBAA HADI OFA YA MAMA IPITE NDIO USHITUKE MWANAO AENDELEE KUZULULA KWENYE VIJIWE VYA MITAANI NA KUKOSA UJUZI
TOTO LANGU LIMEPIGA BUYU SHULENI SIJUI NILIPELEKE WAPI!?
BUYU NDIO NINI TUELEWESHE!?
BUYU NI KUFELI MTIHANI
WEWE WA WAPI NDUGU, HUJUI RAIS WETU DK SAMIA SULUHU HASSAN KAWAPIGA OFA WATOTO 22,000 WOTE WALIOFELI KWA KUPATA ALAMA SIFURI DARASA LA SABA NA KIDATO CHA NNE KUSOMEA KWENYE VYUO VYA UFUNDI
PELEKA BUYU LAKO LIKAPATE ELIMU YA UFUNDI BURE
SHIKA ADABU YAKO MWANANGU SIO BUYU
RAIS WETU ANAHURUMA SANA NA UPENDO KWETU, KIKUBWA KILICHOBAKIA NI KUMUOMBEA DUA KWA MWENYEZI MUNGU AMPE AFYA NJEMA,NGUVU ZAIDI ,MAISHA MAREFU NA MAFANIKIO KATIKA UONGOZI WAKE
HEHEHEH... MASIKINI MBAVU ZANGU JAMANI TARATIBU MSIJE MKASABABISHA NIKAPINDUA GARI KWA KICHEKO

# Tinubu apingwa kwa maandamano

**LAGOS, Nigeria**

MAELFU ya wafuasi wa upinzani nchini Nigeria, wameandamana kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu wa hivi karibuni na kuitaka Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), iandae uchaguzi mwingine.

Waandamanaji hao waliongozwa na mshindi wa pili wa kiti cha urais, Atiku Abubakar wa Chama cha People's Democratic Party, wakiwa wamevalia mavazi meusi huku wakiwa wamebeba mabango.

Habari kutoka Nigeria zilisema waandamanaji walikwenda hadi katika ofisi za INEC na kuzuia lango la kuingia katika ofisi hizo huku wakishinikiza mamlaka ziandae uchaguzi mpya katika mazingira mazuri yatakayoleta matokeo ya haki.

Maandamano hayo yanafanyika wakati vyama vitano vya upinzani nchini humo, vikiwa vimetangaza kupinga matokeo ya uchaguzi vikidai kulikuwa na uchakachuaji.

**Kesi hiyo ilifunguliwa baada mgombea wa chama tawala cha All Progressive Congress (APC), Bola Tinubu...**

Ili kuchaguliwa kuwa Rais wa Nigeria, mgombea anapaswa kupata asilimia 25 ya kura katika angalau theluthi mbili ya majimbo 36 ikiwa ni pamoja na mji mkuu Abuja. Wiki iliyopita, majimbo sita yanayoongozwa na upinzani nchini humo, yaliiomba mahakama ya juu kufuta matokeo ya uchaguzi wa rais kwa madai kuwa Tume ya Uchaguzi ilivunja sheria na kanuni zake wakati wa kuhesabu kura.

Kesi hiyo ilifunguliwa baada mgombea wa chama tawala cha All Progressive Congress (APC), Bola Tinubu, kutangazwa kama mshinda wa urais wa nchi hiyo.

Majimbo ya Adamawa, Akwa Ibom, Bayelsa, Delta, Edo na Sokoto, ndiyo yaliyofungua kesi hiyo. Majimbo hayo yameitaka mahakama kutangaza kuwa matokeo ya uchaguzi wa urais yaliyotangazwa na mwenyekiti wa INEC ni batili na hayana maana yoyote.'

Hakuna majibu ya haraka kuhusu suala hilo kutoka serikalini, kampeni la Tinubu, INEC wala Mwanasheria Mkuu wa Nigeria, Abubakar Malami, ambaye alitajwa kuwa mshtakiwa rasmi katika kesi hiyo.



# Waasi wa M23 washambulia kambi ya jeshi

**KINSHASA, DR Congo**

KUNDI la waasi wa M23 wameishambulia kambi ya kijeshi ya Mubambiro iliyopo nje kidogo na mji wa Goma ambayo inawahifadhi wanajeshi wa Burundi waliowasili nchini humo siku chache zilizopita.

Mashambulizi hayo ya jana yalitokea wakati mapigano makali yalikuwa yakiendelea kati ya jeshi la Kongo na waasi hao kwenye vijiji vya Karuba na Malehe wilayani Masisi, ambako milio ya risasi ilisikika siku nzima.

Taarifa kutoka jeshi la Congo zinaeleza kuwa waasi wa M23 walifyatua maroketi kuelekea kwenye mji wa Sake na kuwauwa watu wawili na wengine kadhaa kujeruhiwa kabla ya kulengwa kwa kambi ya kijeshi Mubambiro iliyopo nje kidogo ya mji wa Goma.

Akizungumza jana, Telesphore Mitondeke ambaye ni mratibu wa shirika la raia wilayani Masisi, alilaani shambulio hilo akieleza kuwa waliolenga nyumba za wakazi na kuongeza hofu mkubwa katika mji huo wa Sake ambao maelfu wameshaukimbia na kuelekea Goma.

Taarifa zinaeleza kuwa waasi wa M23 wametakiwa kuheshimu mkataba wa mwisho wa mkutano mdogo uliofanyika mjini Luanda, Angola uliowakata kurejea katika nafasi yao ya awali kwenye milima ya Sabinyo kuanzia jana, lakini hadi mchana huu waasi hao wamevidhibiti vijiji vya Kibirizi, Kabanda na Kirima katika wilaya ya Rutshuru ambako maelfu wa raia wanahangaika ndani ya msitu.

Uasi wa kundi la M23 umesababisha kuchochea mzozo kati ya Congo na Rwanda, ambapo serikali ya Kinshasa imekuwa ikiutuhumu utawala wa Kigali kuwasaidia waasi hao, shutuma zinazokanushwa vikali na Rwanda.

# Urusi yadaiwa kupoteza wanajeshi Bakhmut

**KYIV, Ukraine**

JUMUIYA ya Kujihami ya Mataifa ya Magharibi (NATO), imedai kuwa Urusi imepoteza wanajeshi mara tano zaidi ya Ukraine katika vita vinavyoendelea mjini Bakhmut.

Ofisa wa NATO ambaye hakutaka jina lake litajwe aliiambia CNN kuwa kulingana na mashirika ya kijasusi ya magharibi, Urusi tayari imepoteza wanajeshi mara tano zaidi karibu na Bakhmut kuliko Ukraine.

Ofisa huyo alisema uchambuzi wa kijasusi katika vita hivyo umeangazia mambo mengi na kwamba licha ya uwiano huu, hasara za Ukraine bado ni kubwa.

Serikali ya Kyiv imekuwa ikitoa taarifa za mara kwa mara kuhusu vita vya Bakhmut ikieleza kuwa, jeshi la Urusi lilipata pigo kubwa kutokana na umahiri wa wanajeshi wa Ukraine.

Taasisi ya Utafiti wa Vita (ISW), pia inabainisha kuwa majaribio ya jeshi la Urusi kuiteka Bakhmut yalipunguza kwa kiasi kikubwa uwezo wake wa kushambulia katika maeneo mengine.

"Jeshi la Urusi lina uwezekano wa kupata ugumu wa kuanzisha mashambulizi mapya katika miezi ijayo," ilieleza ripoti ya ISW.

**BBC**

# Upinzani Uturuki waungana kumpinga Erdogan

**ISTANBUL, Uturuki**

MUUNGANO wa vyama sita nchini Uturuki, umemteua kiongozi wa chama kikuu cha upinzani cha Republican's People's Party (CHP), Kemal Kilicdaroglu, kuwa mgombea atakayepambana na Rais Recep Tayyip Erdogan, katika uchaguzi utakaofanyika Mei 14, mwaka huu.

Hatua hiyo imehitimisha miezi kadhaa ya mifarakano na mivutano iliyokuwa imewavunja moyo wafuasi wa upinzani.

Muafaka huo umefikiwa saa kadhaa baada ya mwanachama muhimu wa muungano huo, Meral Aksener, ambaye anakiongoza chama cha kizalendo cha Iyi na ambaye alikuwa anaupinga uteuzi wa Kilicdaroglu, kukubali suluhisho lililowekwa mezani na kurudi katika muungano huo.

Erdogan ambaye amekuwa kwenye kilele cha siasa za Uturuki tangu mwaka 2003, anakabiliwa na upinzani mkubwa katika uchaguzi ujao, ambao wachambuzi wanasema ndio muhimu zaidi nchini humo kwa muda wa karne nzima.



**Karibu katika duka letu ili kupata bidhaa halisi za Chama Cha mapinduzi**

**Tunauza:**

- Kaunda suti
- Shati
- Tisheti
- Magauni
- Weel cover
- Note book
- kalamu
- viatu
- Kofia
- n.k.

**Mawasiliano**

+255 733 768 825
info@umg.co.tz
www.umg.co.tz

**Tunapatikana**

Ofisi ndogo za CCM Lumumba

Jarida la MWELEKEO

**SOMA NA PAKUA GAZETI HILI BURE**

Kupitia.

www.umg.co.tz




@jaridalamweleko



Mohamed Salah (kulia) ni mchezaji wa kwanza wa Liverpool kufunga hat-trick dhidi ya Manchester United kwenye Uwanja wa Old Trafford tangu, Cristiano Ronaldo alipoichezea Real Madrid mwaka 2003. Picha na BBC

# Liverpool v Man U : Mechi saba za kukumbukwa

**LONDON, England**

TIMU za Liverpool na Manchester United ndiyo klabu mbili zilizofanikiwa zaidi katika mchezo wa soka nchini England na uadui wao mkubwa, umesababisha msururu wa mashindano makubwa kwa miaka mingi.

Kabla ya mechi yao iliyochezwa wikiendi iliyopita Uwanja wa Anfild, ambapo Liverpool ilifanikiwa kuibandika Man United mabao 7-0, tunaangazia baadhi ya mechi kubwa kati ya pande hizo mbili katika enzi ya Ligi Kuu.

**Man Utd 2-1 Liverpool (22 Agosti 2022)**

Mchezo wa hivi majuzi zaidi kati ya pande zote haukua msisimko wa bao la juu kama mingine kwenye orodha hii, lakini ushindi huu ulianza utawala wa Erik ten Hag wa Manchester united.

Kikosi chake kiliingia kwenye mchezo huo baada ya kushindwa kwa mabao 4-0 ugenini dhidi ya Brentford, huku presha ikiongezeka kwa meneja mpya na hisia alihitaji ushindi ili kupata mashabiki upande wake.

United walijibu na kupata ushindi muhimu wa nyumbani dhidi ya wapinzani wao. Jadon Sancho alitangulia kufunga katika kipindi cha kwanza naye, Marcus Rashford akaongeza la pili baada ya kipindi cha mapumziko na kuiweka United katika uongozi.

Mohamed Salah alipunguza nusu ya bao zikiwa zimesalia dakika tisa mchezo kumalizika, lakini Liverpool hawakuweza kupata bao la kusawazisha.

Katika Uwanja wa Old Trafford, Man United ilikua ikitamba na Ten Hag akanyakua ushindi wake wa kwanza wa ushindani kama kocha wa United.

**Man United 0-5 Liverpool (24 Oktoba 2021)**

Mnamo Oktoba 2021, kikosi kikatili cha Jurgen Klopp kiliwafedhehesha wapinzani wao na kuambulia kipigo cha kwanza cha mabao 5-0 kwa United nyumbani tangu Februari 1955.

Mohamed Salah alifunga hat-trick, huku Naby Keita na Diago Jota, pia wakifunga bao wakati kikosi cha Ole Gunner Solskjaer kikibomolewa kwenye uwanja wao wenyewe. United walimaliza wakiwa na wachezaji 10 baada ya Paul Pogba, kutolewa nje baada ya dakika 60 kumkaba Keita, wakati wageni wakiwa tayari wamefunga mabao 5-0. Ulikuwa ushindi wa kuvutia kwa Liverpool huko Old Trafford, lakini kwa United ilikua moja ya mechi ambauo haitaweza kuisahau.

Salah amekuwa mpinzani wa kwanza kufunga hat-trick dhidi ya Man Utd kwenye Uwanja wa Old Trafford tangu Ronaldo, alipoichezea Real Madrid mwaka 2003.

**Man United 3-2 Liverpool (19 Septemba 2010)**

Je, unakumbuka teke la juu la kichwa la Dimitar Berbatov? ufungaji bao wa fowadi huyo wa kustaajabisha uliangaza Old Trafford, alipopiga hat-trick ya ushindi wa mechi kwa msisimko huu.

United na Liverpool waliingia kwenye mechi wakiwa katika hali tofauti, huku timu ya Sir Alex Ferguson ikiwa imeanza msimu vizuri na vijana wa Roy Hodgson, walianza kampeni yao kwa udhaifu.

Wenyeji walichukua nafasi ya kwanza baada ya dakika 42, huku Berbatov, akimalizia mpira wa adhabu uliopigwa na Ryan Giggs. Mshambuliaji huyo raia wa Bulgeria, alifanya mambo kuwa 2-0 muda mfupi kabla ya saa moja kwa mkwaju wake wa sarakasi, kabla ya Liverpool kurejea mchezoni.

Muda wa dakika sita, ambao ulianza kwa mkwaju wa penalti wa Steven Gerrard baada ya Fernando Torres kufanyiwa madhambi kwenye eneo la hatari, ulilegeza kiwango cha wageni, lakini Berbatov ndiye aliyekua na uamuzi wa mwisho.

Katika dakika ya 84, aliinuka juu ya safu ya ulinzi ya Liverpool na kwa mara nyingine tena akamtungua, Pepe Reina kwa kichwa na hivyo kuhitimisha ushindi kwa United.

> Fainali za Kombe la FA zina hulka ya kugonga vichwa vya habari kwa hadithi za kusisimua na kilele cha mashindano ya 1995-1996 haikua tofauti...

**Man Utd 1-4 Liverpool (14 Machi 2009)**

Old Trafford kumekua uwanja wa mapigano kadhaa kati ya United na Liverpool na hii imeonekana kuwa moja ya ushindi bora zaidi wa wageni. United walipata bao la kuongoza kupitia kwa Cristiano Ronaldo baada ya dakika 23, lakini kikosi cha Rafael Benitez kiliambulia patupu.

Fernando Torres alisawazisha dakika tano baadaye kwa mkwaju wa penalti wa Steven Gerrard, ukafanya matokeo kuwa 2-1 kwa Liverpool hadi mapumziko.

Mambo yalizidi kuwa mabaya katika kipindi cha pili kwa United, kwani Nemanja Vidic alitolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kumuangusha Gerrard, kabla ya Fabio Aurelio na Andrea Dossena kukamilisha kipigo hicho ndani ya wiki moja ambapo Liverpool pia waliichabanga Real Madrid 4-0.

**Man Utd 2-1 Liverpool (24 Januari 1999)**

Wakati wa msimu wa 1998-99 na baadaye, mabao ya dakika za mwisho yakawa ada ya Manchester United na pambano hili lilikuwa mfano bora.

Liverpool walitangulia mapema katika pambano la raundi ya nne ya Kombe la FA kwenye Uwanja wa Old Trafford kwa bao lililofungwa na Michael Owen.

Hata hivyo licha ya wageni kushikilia uongozi kwa dakika 85, waliondolewa kwenye michuano hiyo kwa mabao mawili ya haraka-haraka kutoka kwa United kwenye mechi hiyo. Dwight Yorke na Ole Gunnar Solskjaer, walipata ushindi kwa United kwa mabao katika dakika mbili za mwisho na kuhakikisha timu ya Sir Alex Ferguson, inasonga mbele katika raundi inayofuata.

Wangeenda kukamilisha Treble ya kihistoria huku, Solskjaer akifunga bao muhimu zaidi la dakika za mwisho kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa.

**Man Utd 1-0 Liverpool (11 Mei 1996)**

Fainali za Kombe la FA zina hulka ya kugonga vichwa vya habari kwa hadithi za kusisimua na kilele cha mashindano ya 1995-1996 haikua tofauti.

Wapinzani hawa wa zamani, walichuana kwenye uwanja mkubwa wa soka ya Uingereza, Wembley.

Kwa kiasi kikubwa, mchezo wenyewe haukua wa kusisimua, zaidi ya wakati wa kichawi ambao uliipatia ushindi timu ya Sir Alex Ferguson. Zikiwa zimesalia dakika nne na mechi ya mwisho ikionekana kukaribia muda wa nyongeza, Eric Cantona alipata nafasi kwenye eneo la goli na kuupiga mpira kupitia msitu wa miili na kuifungia United bao la ushindi. Mfaransa huyo alionekana kuwa tofauti kwa Mashetani Wekundu, kama ilivyokua mara nyingi wakati alipokuwa Manchester.

**Liverpool 3-3 Man Utd (4 Januari 1994)**

Lilikuwa ni pambano la Waskochi dimbani, huku vijana wa Sir Alex Ferguson wakifurahia maisha kileleni mwa msimamo la Ligi Kuu walipokwenda Anfield, kumenyana na Liverpool ya Graeme Souness.

Viongozi wa ligi walisonga mbele mapema pale, Steve Bruce alipofungua ukurasa wa mabao zikiwa zimesalia dakika tisa mpira kumalizika. United walikua mbele kwa mabao 3-0 baada ya dakika 24 pekee, huku Ryan Giggs na Denis Irwin pia wakiwa kwenye orodha ya wafungaji mabao na walionekana kuondoka na ushindi.

**Lakini Liverpool hawakutaka kulazwa Anfield.**

Nigel Clough alifunga mabao mawili kabla ya muda wa mapumziko na kupunguza idadi ya mabao na baada ya kipindi kigumu cha pili, wenyeji walisawazisha kupitia kwa Neil Ruddock dakika ya 79 kwa kichwa na kukamilisha moja ya marudiano ya kukumbukwa katika Ligi Kuu ya England.

**Kwa hisani ya BBC**

# Burudani



LONDON, England

NAHODHA wa Manchester United, Bruno Fernandes amesema kuwa ameumizwa na kipigo cha mabao 7-0 ilichopata dhidi ya Liverpool katika Uwanja wa Anfield.

Kiungo huyo ambaye alikua miongoni mwa mastaa wa Man United waliocheza kwa kiwango cha chini, alisema matokeo hayo ni mabaya na hayakubaliki.

Katika mchezo huo, Fernandes alitumia muda mrefu zaidi kulaumu ndani ya uwanja kitendo ambacho kilidhoofisha sehemu ya kiungo.

"Tumechanganyikiwa. Hakika haya ni matokeo mabaya zaidi, tulikuja hapa (Anfield) tukiwa na matumaini lakini hali ikawa tofauti.

"Kipindi cha kwanza tulicheza kwa kiwango bora, kwa kweli tulihimili sehemu ya mchezo, dakika 45 za pili hali ilikua mbaya, tulishindwa kulinda ubora wetu," alisema mchezaji huyo.

Kiungo huyo alisema, walicheza kwa kuacha nafasi kubwa kitendo ambacho kilitoa mwanya kwa Liverpool kucheza kwa ufanisi.

Alisema walipambana kuweka usawa wa mchezo, lakini walishindwa kuhimili kasi ya wapinzani wao hivyo mechi ilikua ngumu kwa upande wao.

Matokeo hayo yamewashtua mashabiki na wachezaji wa Man United duniani kwa kuwa hawakutarajia timu hiyo ya Old Trafford kupata kipigo hicho.



## Wamoto Music kuachia kibao kipya cha Baby

Na Mwandishi Wetu

BAADA ya kutamba na nyimbo kadhaa za singeli, wasanii wa Singeli Wamoto Music wanakuja na kibao kipya kiitwacho Baby.

Kwa mujibu wa ukurasa wa Instagram, wasanii hao wamejipanga kuachia kibao hicho ndani ya mwaka huu huku wakiwataka wadau wa muziki kukaa mkao wa kula. "Waiting is over!!!Leo ndo leo wamotomusic aka fire girls, tutaachia audio yetu mpya yenye kukata kiu ya mashabiki zetu iitwayo Baby," ilisema taarifa ya uongozi wa wasanii hao. Wamoto wataachia wimbo huo, baada ya kufanya vizuri na ngoma kadhaa kama Wanyooshe, Mume, Sijaona pamoja na nyingine nyingi.



## Makabila awatupia dongo wasanii wasiojitambua

Na Mwandishi Wetu

MSANII wa muziki wa singeli, Dulla Makabila amesema suala la wasanii wa muziki huo kuwa wanalipwa pesa kidogo si la kweli, bali wasanii wasiojitambua ndiyo wanalipwa pesa ndogo.

Makabila aliyasema hayo alipokua kwenye 'listening part' ya albamu ya Kayumba iliyofanyika Uncle's Masaki jijini Dar es Salaam.

"Natamani hata niwataje majina hawa wasanii wasiojitambua, maana wananikata kweli, mimi utakuta nimekataa labda kiasi fulani cha hela kutoka kwa promota, lakini unashangaa mwenzako amechukua amekwenda," alisema Makabila.

Makabila alisema, wasanii wengi wa singeli wanaofanya hivyo, hawana vyanzo vingine vya mapato hivyo kujikuta wakichukua kiasi chochote cha pesa jambo ambalo linawashushia hadhi yao, ambayo yeye anapambana kuipandisha.

## Rayvanny amtakia heri Paula Kajala

Na Mwandishi Wetu

MSANII wa muziki wa kizazi kipya nchini, Rayvanny ameoneka ukomavu wa akili, baada ya kumtakia heri aliyekua mpenzi wake, Paula Kajala kheri baada ya binti huyo kudokeza kwamba ameolewa. Kupitia ukurasa wake wa Facebook, Rayvanny alipakia picha ya Paula akiwa anavishwa pete na mwanamume kwa jina Ally na kumpa hongera kwa hatua hiyo, ambayo ni ndoto kwa kila mwanamke.

"Hongera sana P... na iwe heri," Rayvanny aliandika kwenye picha hiyo na kupokelewa kwa maoni mseto kutoka kwa maelfu ya mashabiki wake mtandaoni.



Hata hivyo ndoa ya Paula, imezua vijembe mitandaoni, idadi kubwa ya watu wakionekana kutoamini kama kweli ni ndoa au ni kiki tu anafukuzia suala la harusi.

Mrembo huyo ambaye ni mtoto wa pekee wa Kajala Masanja, kutoka familia ya Kikristo alipakia picha akiwa anavishwa pete ka kutokana na picha hizo ni dhahiri kwamba ni ndoa ya Kiislamu. Hata hivyo hakuonesha uso wala sura ya mwanaume huyo Ally, jambo ambalo lilizidisha kutoamini kutoka kwa wengi wa wanamitandao.

# ZFF yazitaka timu za Ligi Kuu kuwa na ushindani

**Na Mwandishi Wetu**



RAIS wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), Abdullatif Ali Yasin (pichani) amezitaka klabu zinazoshiriki ligi visiwani Zanzibar kuendelea kuwa na ushindani, ili kuhakikisha anapatikana bingwa ambaye ataiwakilisha nchi vizuri.

Yasin aliyasema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati akifungua droo ya upangaji wa ratiba ya michuano ya Kombe la Shirikisho {FA}, iliyofanyika katika ukumbi wa mkutano wa shirikisho hilo uliopo Uwanja wa Amaan mjini hapa.

Alisema shirikisho lao pamoja na mambo mengine, lipo kwa ajili ya kuona mchezo wa soka unakua na kukuza vipaji vya vijana.

Rais huyo alisema mpango huo unaenda sambamba na juhudi za serikali pamoja na kumuunga mkono Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

"Tupo kwenye malengo ya rais ya kuukuza mchezo huu, nawashukuru wadau kwa kuheshimu taratibu zote ambazo ZFF imekuwa ikizifanya katika kuuendeleza mchezo huu," alisema.

Alisema kitendo cha wadau hao kujitokeza kwa wingi na kufuata wito wa shirikisho hilo, kinaonesha wazi jinsi ambavyo wametilia maanani mambo yote ambayo yanafanyika ndani ya ZFF.

Awali Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Ali Bakar Cheupe alisema upangaji wa droo hiyo kwa ajili ya michuano hiyo, utakua ni endelevu na kuzishirikisha klabu kwa kila wanapomaliza hatua moja.

Alisema michuano hiyo, ambayo inaingia katika hatua ya pili imepangwa kuendelea Machi 16 mwaka huu na kushirikisha timu 32 zote za Unguja na kwa Pemba nako watakua na michuano yao inayoshirikisha timu 16.

Kwa mujibu wa Cheupe, bingwa wa FA atapatikana kwa kuwakutanisha mabingwa wa Unguja na Pemba, ambao mshindi atapata sh. milioni 30 zilizotolewa na Benki ya Watu wa Zanzibar.

# Leo zamu ya Yanga, yaita mashabiki kuona 'pira sukari'

Inatoka Uk.24

litakalofungwa na timu hiyo atatoa sh. milioi 5, hivyo wanatarajia kurudisha furaha kwa rais kwa kutoka na ushindi uwanjani.

Pia aliwataka wanawake kufika kwa wingi uwanjani, ili kusherehekea Siku ya Wanawake huku wakipata burudani ya nguvu 'pira sukari', kutoka kwa wachezaji wao ambao wameahidi ushindi mnono ili kujiwekea mazingira mazuri ya kucheza robo fainali.

Kamwe alisema maandalizi yako vizuri ndani na nje ya uwanja, hakuna mchezaji aliyepata majeruha na kila mmoja ana morali ya kushinda mechi ya leo, hivyo amewataka mashabiki kujitokeza mara mbili ya walivyojitokeza walivyocheza na timu ya TP Mazembe Congo.

"Wachezaji wamesema katika mechi waliyocheza na TP Mazembe Uwanja wa Mkapa, walipata nguvu kubwa na kupata ushindi wa mabao 3-1 baada ya kuona mashabiki wengi wamejitokeza kuwashangilia, hivyo mechi na Bamako wameomba wajitokeze mara mbili zaidi ili kuwapa nguvu," alisema.

Alisema lengo lao kubwa ni kwenda kucheza nusu fainali ya michuano hiyo ya Shirikisho kwa kuwa ndoto yao kubwa ni kufika mbali na si kuishia hatua ya makundi na ndiyo maana wamejiandaa vya kutosha.

"'Vibe' litaanzia pale nje kwa Mkapa kuanzia saa 10 jioni ambapo tunamleta DJ mkubwa anayetamba kwa sasa hapa nchini, hivyo mashabiki wataanza kupata uhondo kuanzia muda huo hadi saa 12 kabla ya mechi kuanza, vilevile wakati wa mapumziko shangwe zitaendelea tena hivyo tunawaomba mashabiki wetu mje kwa wingi," alisema.



Mchezaji wa Arsenal, Reiss Nelson {katikati} akishangilia na wachezaji wenzake mara baada ya kuifungia timu yake bao la tatu na la ushindi dhidi ya Bournamaouth FC wakati wa mechi ya Ligi Kuu ya England iliyochezwa Uwanja wa Emirates jijini London mwishoni mwa wiki. Katika mechi hiyo Arsenal ilishinda mabao 3-2. Picha na Mtandao

# Guardiola aitaja Arsenal kuwa timu bora msimu huu

**MANCHESTER, England**

KOCHA Mkuu wa Manchester City, Pep Guardiola ameitaja Arsenal kama timu bora msimu huu ndani ya Ligi Kuu England, ikiwa timu yake katika kuwania ubingwa.

Arsenal wapo juu ya msimamo wa ligi, wakiifunika Man City iliyo nafasi ya pili ambapo timu hizo zipo tofauti ya pointi tano. Msimu huu, Arsenal wanapambana kusaka taji hilo ambalo mara ya mwisho walilibeba mwaka 2003/04, huku msimu wa 2015/16 wakimaliza nafasi ya pili.

Bosi huyo wa Man City, alisema anafikiria kuwa Arsenal ndiyo timu bora ndani ya ligi hiyo msimu huu kutokana na mwenendo wake.

"Kwa sasa wao wamekuwa tishio, wamekuwa na mabadiliko, kwenye mipira ya kutengwa wako vizuri, ndiyo maana kwangu naona wao ni timu bora.

"Hawajakua nafasi za juu nne bora kwa muda mrefu na ilikua kama wanahitaji muda, lakini kwa sasa wako vizuri, msimu huu wamejipanga.

"Kile ambacho wanakifanya Arsenal kwa sasa, kila mmoja anakiona, hakuna siri," alisema Guardiola.

# Reiss Nelson angepotea kabla hata hajakomaa kwa Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI kinda wa Arsenal, Reiss Nelson dakika za majeruhi alisimama pembeni ya kibendera cha kupigia kona kama vile amejitenga na zile purukushani za kuusubiri mpira wakati wa mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Bournemouth FC iliyochezwa wikiendi iliyopita.

Ubao wa matangazo ukisomeka Arsenal 2 Bournemouth 2 na ikiwa ni dakika ya 97, muda wowote ule mwamuzi angepuliza filimbi ya kumalizika kwa mechi.

Beki alipouokoa mpira kwa kichwa ukatua miguuni mwa Nelson, aliyeutuliza kwa kifua na kufumua shuti lililokwenda moja kwa moja kimiani.

Shangwe ikalipuka baada ya goli la tatu kufungwa na uwanja mzima ukajawa na furaha isiyoelezeka. Ni ushindi wa jasho kweli kweli.

Pointi tatu zilizohangaikiwa kwa dakika zote 90 na zile sita za nyongeza. Kamera ilimuonesha kocha, Mikel Arteta pembeni ya uwanja akimuuliza mwamuzi wa akiba zitaongezwa dakika ngapi kwa ishara ya vidole.

Uso wake umejawa na wasiwasi akikumbuka kuwa sare ya aina yoyote ingewapa Arsenal uongozi wa pointi tatu badala ya tano, nyuma ya Man City wenye timu yenye uwezo wa kutafuta ushindi wa kuvutia au ule wa kusaka tu pointi tatu zisizo na mvuto.

Bao la Nelson lilimaanisha kuwa pointi zinazotofautisha hizi timu mbili za juu ni zile zile tano. Ahueni angalau wa mzunguko mmoja wa mechi za Ligi Kuu kwa upande wa Arsenal inayoongoza sehemu kubwa ya msimu huu.

Kila mchezaji wa Arsenal akamzunguka, Nelson na kumpongeza kwa bao lake lililoamua mchezo jioni ile. Ni mchezaji mwenye historia zinazofanana na zile za wanasoka wengi wa Uingereza.

Anapelekwa na wazazi au walezi wake na kukabidhiwa kwa uongozi wa klabu akiwa mtoto wa miaka tisa.

Picha ya ukumbusho inapigwa yenye kumuonesha akiwa na kalamu mkononi na makaratasi ya mikataba mezani na nyuma wanaonekana viongozi wa timu inayokabidhiwa mtoto pamoja na wazazi wake. Anakua ni mali ya timu husika.

Wamelelewa mamia ya wachezaji wa kizungu kwa mtindo huu. Timu za Ulaya hazipokei watoto wanaokwenda viwanjani kwa kutoroka majumbani mwao kama baadhi ya timu zetu.

Kila kitu kinafanyika katika msingi wa maandishi.

Kwamba tarehe ya mwezi fulani na mwaka fulani, mtoto wao akiwa na miaka tisa au kumi amekabidhiwa kwa uongozi wa klabu.

Yanga na Simba wanashindwa kulea vijana tangu wakiwa na umri mdogo. Ni tamaa zao zinazowasumbua. Wanamuona mchezaji kijana anayetamba katika kikosi fulani na wanaanza kumfukuzia kwa njia mbalimbali.

Anapokuja katika klabu yao, wanajikuta wakimsahau mchezaji kijana ambaye pengine anao uwezo hata kumzidi huyo nyota anayetamba midomoni mwa watu.

Miaka yote wanakuwa na timu zenye kutaka kusajili wachezaji wanaowachukua katika klabu nyingine na kushindwa kuwa na muendelezo wa malezi wa timu zao wenyewe.

Yanga angalau wamepata ujasiri wa kudumu na Clement Mzize. Na hasa anafunga magoli, hivyo wanashindwa kumlaumu au kuhoji maamuzi ya makocha ya kumuamini.

Angekua hafungi mara kwa mara, hakuna shabiki au kiongozi angeweza kumvumilia kucheza mechi ya ushindani.

Na timu za Ulaya zinatushinda katika muundo wa michuano yao mbalimbali, hasa ile inayochezwa sambamba na mechi za Ligi Kuu.

Reiss Nelson, mara nyingi anatokea benchi lakini haonekani kuwa na tofauti sana na wachezaji wanaozoea mechi za kikosi cha kwanza. Michuano ni mingi inayowapa uzoefu na nafasi ya kutunza viwango vyao.



## Wamoto Music kuachia kibao kipya cha Baby
Uk. 22

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Mwelekeo Spoti

| Jumanne Machi 8 - 14, 2013 |



## Guardiola aitaja Arsenal kuwa timu bora msimu huu
Uk. 23

# Simba yaibamiza Vipers na kufufua matumaini

**Na Mwandishi Wetu**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika michuano ya Klabu Bingwa Afrrika Simba jana walifufua matumaini kucheza hatua robo fainali ya michuano hiyo Kundi C baada ya kuifunga Vipers ya Uganda bao 1-0 katika mechi iliyochezwa Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam. Kwa matokeo hayo Simba imefikisha pointi ikishika nafasi ya pili nyuma Raja Casablanca yenye pointing 12 baada ya kuifunga Horoya mabao 3-1.

Mpira ulianza kwa timu zote kucheza kwa kutegeana ambapo Vipers ndio walioanza kulifikia lango la Simba baada kipa Aishi Manula kupangua shut kali na kuwa ambayo haikuzaa matunda.

Bao la Simba lilipatikana dakika ya 45 lililowekwa kimiani na Clotus Chama ambaye alipokea pasi kutoka kwa Sadio Kanuti.

Kipindi cha pili kama Simba wangekuwa makini wangeweza kuondoka na ushindi mnono huku kipa wa Vipers akiondoa michomo Mingi kutoka kwa Chama aliyekuwa nyota wa mchezo pamoja Saido Ntibazonkiza.






Mayele

# ...Leo zamu ya Yanga, yaita mashabiki kuona 'pira sukari'

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Klabu ya Yanga, umewataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kufika uwanjani kwa wingi katika mechi ya Kundi D Kombe la Shirikisho Afrika, itakayopigwa leo Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam dhidi ya Real Bamako ya Mali kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani pamoja na kuangalia burudani murua ya soka itakayooneshwa na timu hiyo.

Katika mechi ya awali, Yanga walilazimishwa sare ya bao 1-1 na Real Bamako iliyochezwa Uwanja wa Machi 26 jijini Bamako nchini Mali. Yanga walitangulia na bao la mshambuliaji raia wa DR Congo, Fiston Kalala Mayele dakika ya 60 kabla ya beki mzawa, Emile Kone kuisawazishia Bamako dakika ya 90.

AKizungumza Dar es Salaam jana Msemaji wa Yanga, Ally Kamwe alisema leo ni siku kubwa mno kwa wanawake katika Uwanja wa Benjamini Mkapa, kwanza kabisa ni Siku ya Wanawake Duniani akiwemo Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ameahidi kila bao

Inaendelea Uk.23

## Serikali yashauriwa kuwekeza nguvu soka la wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar {SMZ}, imeshauriwa iwekeze nguvu katika soka la wanawake ili na wao waweze kuonesha vipaji, vitakavyovutia kupata timu bora kuendesha maisha yao.

Ushauri huo ulitolewa na Kocha Mkuu wa timu ya PDS Princes, Khalid Khamis Suleiman alipozungumza na mwandishi wa habari hizi katika ofisi ya timu hizo Kibele Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema soka la wanawake kwa sasa duniani sasa hivi ndiyo kitu ambacho, kimepewa kipaumbele na serikali zao zimekua zikiwekeza kupitia mpira huo.

Kocha huyo alisema, kutokana na umuhimu huo kama taasisi ambayo inajishughulisha na kukuza vipaji vya vijana kupitia vitu tofauti, ndiyo maana na wao wakaunda timu hiyo kwa lengo la kutengeneza ajira kwa wasichana.

"Ulimwenguni mpira wa miguu ni dili, lakini kwa kwetu bado na imekua shida na tunahisi serikali haijatilia mkazo juu ya suala hilo," alisema kocha huyo.

Alisema ameamua kusema hivyo, kutokana na mambo ambayo wamekuwa wakifanyiwa kama timu za wanawake wakati wanapokwenda kucheza.

## Reiss Nelson angepotea kabla hata hajakomaa kwa Tanzania
Uk. 23



Nelson